
SportPesa
TZS. 537,737,060
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Ajinyonga** hadi kufa, otoa sababu kuwa ni msongo wa mawazo

UKURASA 4


ama
AFYA NA MAZINGIRA
Unatumia tumbaku? Zijue sumu zake zinavyojificha mwilini na kukumaliza
Magonjwa yasiyoambukiza yalivyo hatari kwa binadamu
Atembea Kigoma hadi K'njaro kampeni ya chanjo UVIKO 19
•Mwanariadha aliyepatiwa cheti na wizara

UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Septemba 30, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580718
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## KESI YA MBOWE

# Aeleza alivyomtafuta mume hadi mochwari

UKURASA 2



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (kulia) na wenzake wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 3

### OLE NASHA KUZIKWA ARUSHA JUMAMOSI

MAZIKO ya aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, William Ole Nasha, yanatarajiwa kufanyika Oktoba 2, mwaka huu, kijijini kwake Osinoni, mkoani Arusha. Aidha, leo itafanyika ibada ya kuaga mwili katika ...

UKURASA WA 4

### MASHAHIDI ZAIDI JAMHURI KUTOA USHAHIDI KESI YA SABAYA

KESI ya uhujumu uchumi namba 27, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita, inatarajiwa...

UKURASA WA 17

### MWINYI ASEMA SERIKALI HAINA UKABILA WALA DINI

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa anaiendesha Serikali ya Zanzibar bila ya ubaguzi wa kidini, rangi wala kabila na kwa kufuata misingi...

## Mchakato Chato kuwa mkoa sasa wakamilika

UKURASA 2



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa (katikati), akiangalia mzoga wa chui aliyeuawa baada ya kuvamia makazi ya watu eneo la mji mdogo wa Bomang'ombe, wilayani Hai, mkoani humo jana na kuleta taharuki. PICHA: MARY MOSHA

## Gari la mbunge CCM lachomwa moto na watu wasiojulikana

UKURASA 2

**MICHEZO** **BIASHARA UNITED YAMULIKA PIA CAF** UK.20

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Aeleza alivyomtafuta mume hadi mochwari

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa tatu katika kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, Lilian Kibona, amedai alimtafuta mumewe vituo vinne vya polisi, wodini na mochwari za hospitali tatu bila kumwona.

Lilian (25) ambaye ni mke wa mshtakiwa wa pili, Adam Kasekwa, alidai hayo Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Mustapha Siyani akiongozwa na Wakili John Mallya.

Alidai wakati anaolewa mwaka 2016, Kasekwa alikuwa askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Kikosi cha Ngerengere na baada ya kuachishwa jeshi, aliendelea kufanya shughuli binafsi za biashara.

Alidai mwanzoni mwa Agosti, 2020 kulikuwa na mawasiliano kati ya Kasweka na rafiki yake Mohammed Ling'wenya, alimfahamisha kuna kazi Moshi, hivyo atampitia Chalinze ili waende.

Shahidi huyo alidai kuwa mume wake alimshirikisha taarifa hizo na yeye kama mke alimruhusu aende, lakini kabla ya safari walikwenda Morogoro na waliporudi wakaenda Moshi na walipofika alimjulisha kwamba amefika na mawasiliano yalikuwa mazuri kati yao.

"Agosti 5, 2020 muda wa saa 1:00 asubuhi alinipigia simu kunijulia hali na mtoto lakini kabla ya kuendelea na mazungumzo aliniambia nisubiri kidogo atanipigia baadaye.

"Nilipoona hajapiga niliamua kumpigia, lakini simu iliita kwa muda mrefu bila kupokewa na baadaye ilipokewa na hakuna aliyeongea upande wa pili na baadaye ikawa haipatikani," alidai.

Lillian alidai kuwa hakupigiwa tena mpaka alipoamua kumpigia Ling'wenya ambaye naye simu yake haipokewa hadi siku ya pili alipojaribu kupiga tena, lakini haikuwa hewani.

"Agosti 9, 2020 ilikuwa siku ya Jumapili niliamka mtoto akiwa anasumbuliwa na tumbo, hivyo nikampeleka Hospitali ya Serikali Chalinze, akapatiwa matibabu na kurudi nyumbani ambapo nilikuta alama za nyayo za watu mlangoni na mlango ukiwa wazi, kitasa kimevunjwa wakati nilicha umefungwa.

"Wazo la kwanza nilidhani ni wezi, lakini nilipoingia ndani kwa haraka haraka sebuleni vitu kama TV vilikuwapo. Nilipokwenda chumbani nilikuta nguo zote kwenye mabegi zimemwagwa na begi moja la Kasekwa alilotoka nalo Congo lenye mabaka ya jeshi limechukuliwa.

"Niliamua kwenda kwa jirani akanifahamisha kwamba kuna magari ya polisi yakiwa na askari waliovaa sare na wengine kiraia ambao waliingia ndani na kuanza kupekua. "Alisema waliondoka na begi, vyeti vya kijeshi vya Kasekwa, hati ya kiwanja na kadi ya pikipiki.

"Mkuu wa Upelelezi wa Chalinze aliacha namba yake ya simu ili kama kuna lolote nimpigie kwa ufafanuzi zaidi. Nilipompigia aliniambia alipokea simu kutoka Polisi Moshi ambao walimtaka aongozane nao kufanya upekuzi nyumbani kwa Kasekwa," alidai.

Shahidi aliendelea kudai kuwa alimtafuta mke wa Ling'wenya ambaye alimwambia wamtafute mke wa Bwire kwa sababu wote walikuwa na sintofahamu ya wapi walipo waume zao.

Baada ya kupata mawasiliano ya mke wa Bwire alimshauri wakutane Dar es Salaam baada ya mke wa Ling'wenya kupata taarifa kuwa waume zao walipelekwa huko.

Alidai walipowasili Dar es Salaam alifika nyumbani kwa mke wa Bwire, Temeke ambako walishauriana kuanza kuwatafuta waume zao katika vituo vya Polisi vinne na hospitali tatu.

Alivitaja vituo hivyo kuwa ni Chang'ombe, Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam, Kituo cha Polisi Oysterbay na Kituo cha Polisi cha TAZARA ambavyo waliangalia majina yao kwenye vitabu vya kumbukumbu, lakini hayakuwapo ndipo walipoamua kwenda kuwatafuta katika wodi na vyumba vya kuhifadhia maiti katika Hospitali za Muhimbili, Mwananyamala na Amana ambako hawakuwaona pia.

Alidai kuwa akiwa na wenzie waliangalia miili yote mochwari bila mafanikio na baada ya hapo alirudi Chalinze bila kujua alipo mume wake mpaka Agosti 19, 2020 alipoona kwenye taarifa ya habari katika kituo cha televisheni cha ITV akiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akishtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi na ugaidi.

Lilian anadai aliwahi kwenda kumuona Gereza la Segerea, alimfahamisha kuwa alipigwa na kwa kumwangalia aliona amekonda hadi macho yake yakiwa yameingia ndani.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfani Bwire, Kasekwa na Ling'wenya ambao wanakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo kula njama na kufanya vitendo vya kigaidi.

UAMUZI OKTOBA 19

Mahakama inatarajia kutoa uamuzi katika shauri dogo la kupinga kupokelewa kwa maelezo ya onyo ya mshtakiwa Adamu Kasekwa kwa madai aliteswa kabla na wakati akichukuliwa maelezo hayo Oktoba 19 mwaka huu.

Pia mahakama hiyo itatoa uamuzi wa endapo maelezo hayo yalichukuliwa zaidi ya saa nne inayoruhusiwa kisheria.

Jaji Siyani alifikia uamuzi huo baada ya upande wa utetezi kufunga ushahidi wakiwa na mashahidi watatu na kuomba kufanya majumuisho ya mwisho kwa maandishi Oktoba 4, mwaka huu.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, alikubali maombi ya upande wa utetezi na mahakama iliwaruhusu kuwasilisha hoja zao kwa ufupi zikiwa na mambo muhimu na zisizozidi kurasa tano Oktoba 4, mwaka huu.

Mahakama hiyo ilielekeza majumuisho hayo kuwasilishwa kwa msajili, yatakapomfikia Jaji Siyani atatoa uamuzi Oktoba 19, mwaka huu.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (kushoto), akizungumza na Katibu Mkuu wa Chama cha Frelimo cha nchini Msumbiji, Roque Silva Samwel, baada ya mazungumzo yao katika ofisi ndogo za makao makuu ya CCM Lumumba, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Walichoma moto gari la mbunge

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

WATU wasiojulikana wamelichoma moto gari la Mbunge wa Mbozi kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), George Mwenisongole na kuliteketeza kabisa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Jane Magomi, akizungumza na gazeti hili jana kwa simu, alisema tukio hilo lilitokea jana saa 9:00 usiku nyumbani kwao mbunge huyo eneo la Ichenjezya Vwawa Mjini wilayani Mbozi.

Kamanda Magoni alisema polisi walipata taarifa za kuteketea gari aina ya Toyota Brevis yenye namba T. 231DDZ mali ya mbunge huyo, na kwamba walifika eneo la tukio wakiwa na Jeshi la Zimamoto na kufanikiwa kuuzima ili moto usilete madhara katika nyumba.

Alisema sababu za kuchomwa moto gari hilo hazijajulikana, lakini polisi wanaendelea na uchunguzi kubaini na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kuwabaini wahusika.

Kufuatia tukio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba ametoa salamu za pole kwa mbunge huyo.

Mgumba alitoa wito kwa wananchi kutulia na kuwa na subira katika kipindi hiki na kuacha kutoa taarifa kwa watu wasiohusika.

Mbunge Mwenisomgole alisema tukio hilo limemsikitisha na kwamba kwa sasa ni mapema kuzungumzia jambo hilo.

"Kwa kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vimeanza kuchunguza tukio hilo, nafikiri tuviachie vifanye kazi yake na baada ya uchunguzi ukweli utajulikana," alisema.

# Mchakato mkoa Chato wakamilika

**Na Richard Makore,** MWANZA

MCHAKATO wa kuifanya Wilaya ya Chato kuwa mkoa umekamilika na kinachosubiriwa kwa sasa ni majibu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuhusu utata wa Wilaya ya Busanda ibaki katika mkoa gani.

Kikao cha Kamati ya Ushauri mkoani Geita (RCC), tayari kimeridhia kuanzishwa kwa mkoa mpya wa Chato na wilaya zitakazounda mkoa huo zimetangazwa.

Wilaya hizo ni pamoja na Bukombe, Chato, Kakonko, Bihalamulo, Ngara, pamoja na Busanda ambayo inabishaniwa na pande mbili kati ya Geita na Chato iwe upande gani na kulazimika suala hilo kupelekwa TAMISEMI ili kutolewa uamuzi.

Akiongoza kikao cha RCC hivi karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Sinyamure, alitangaza kukamilika kwa mchakato huo na kwamba kinachosubiriwa kwa sasa ni uamuzi kuhusu Wilaya ya Busanda iwe mkoa gani.

Mchakato huo ulianza muda mrefu kabla aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, John Magufuli hajafariki dunia mapema mwaka huu.

Magufuli aliwahi pia kuwa mbunge wa Jimbo la Chato kwa miaka 20.

Wakati mchakato huo wa kuanzisha mkoa mpya wa Chato, ukikamilika, Kikao cha Kamati ya Ushauri (RCC), mkoani Mwanza juzi kikiridhia kuhamishwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa iliyokuwa mkoani humo kwenda mkoani Geita.

## Nasha kuagwa Dodoma leo, kuzikwa Arusha Jumamosi

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

MAZIKO ya aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, William Ole Nasha, yanatarajiwa kufanyika Oktoba 2, mwaka huu, kijijini kwake Osinoni, mkoani Arusha.

Aidha, leo itafanyika ibada ya kuaga mwili katika viwanja vya Bunge, kwa ajili ya kusafirishwa kwenda mkoani humo.

Akitoa ratiba ya mazishi kwa waandishi wa habari jijini hapa jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema baada ya vikao vya pamoja kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na familia wamekubaliana azikwe Jumamosi.

Alisema serikali inaendelea kufanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha taratibu za mazishi na maziko zinafanyika kwa heshima zote.

Mhagama alisema mwili wake utaagwa, kwenye viwanja vya Bunge kuanza saa tano ya subuhi na baada ya hapo utasafirishwa kwenda Arusha.

Hata hivyo, Waziri Mhagama alisema vikao vinaendelea, ili kuhakikisha ratiba hiyo inafuatwa kwa kushirikiana na familia.

Kwa upande wake, Msemaji wa familia, Edward Porokwa, alisema wanafarijika sana kwa ushirikiano wanaopata kutoka serikalini.

Kaporokwa aliishukuru serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa utaratibu uliochukuliwa kwa kuhakikisha wanaupeleka mwili wa ndugu yao kuzikwa kijijini kwake kwa heshima zote.

# Mwigulu amwagiza CAG uchunguzi halmashauri 4, taasisi

**Josephine Majura na Alice Nyange**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amemwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuzifanyia ukaguzi na uchunguzi wa kina halmashauri 4 za wilaya na taasisi moja ya serikali kwa kukiuka Sheria za Ununuzi wa Umma.

Alitoa maagizo hayo baada ya kupokea Ripoti ya Tathmini ya Utendaji ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, jijini Dodoma. Dk. Mwigulu amesema uchunguzi lazima ufanyike ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa watu wote watakaobainika kukiuka taratibu za ununuzi ikiwamo kutoa zabuni nje ya mfumo wa kielektroniki wa TANePS unaotumika kuchakata zabuni.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mjumbe wa Bodi ya PPRA, Prof. Ninatubu Lema kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Marten Lumbanga, Taasisi tano zilizopata wastani hafifu wa kufuata sheria taratibu na kanuni za ununuzi wa umma kuwa ni Halmashauri ya Mji Kondoa, Halmashauri ya Mbogwe, Halmashauri ya Biharamulo, Halmashauri ya Chato na Taasisi ya Utafiti wa Wanyama.

Aidha, Dk. alimuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, kuziandikia waraka Taasisi 172 ambazo zimeunganishwa kwenye Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Mtandao (TANePS) watoe sababu za kutotumia mfumo huo katika kufanya ununuzi.

Alizitaka pia Taasisi nunuzi zote kutumia asilimia 30 ya gharama yote ya zabuni zinazotangazwa katika mpango wao wa ununuzi wa mwaka kwa ajili ya kuyawezesha makundi maalumu yakiwamo ya vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa sheria ya ununuzi.

"Nimesikitika sana baada ya kusikia kwamba kati ya Taasisi 86 mlizozikagua ni Taasisi mbili tu ndizo zilitenga asilimia 30 katika mpango wao wa ununuzi wa mwaka kwa ajili ya makundi maalumu," alisisitiza Dk. Mwigulu.

Prof. Lema, alisema katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 walifanya ukaguzi wa mikataba 8,838 ya ununuzi yenye thamani ya Sh. trilioni 9.2 kutoka Taasisi 86.

Prof. Lema alifafanua kuwa matokeo ya ukaguzi huo yalionyesha Taasisi 130 kati ya 718 zilizounganishwa kwenye mfumo wa Ununuzi wa TANePS hazikuwasilisha mipango yao ya ununuzi kupitia mfumo huo huku Taasisi 208 ziliwasilisha mipango yao kupitia mfumo huo lakini zikachakata zabuni nje ya mfumo hali inayoashiria kuwapo kwa vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka.


## Ushauri wa Wadau wa Mitaa kwa shughuli za mradi wa kaboni ya Dhahabu 'RUDI WATER Project'

4ife

**Ndugu Mdau,**

4LIFE Solutions itatekeleza shughuli za mradi wa kaboni VPA2: 'RUDI WATER Project' chini ya Mpango wa Shughuli za Kiwango cha Dhahabu (PoA) Programu endelevu ya Usafi wa Maji. Mradi utasambaza teknolojia salama ya utakaso wa maji, inayoitwa SaWa, kulingana na Teknolojia inayotumia miale ya jua ili Kuzuia Maambukizi ya magonjwaa/maambukizi yanayotokana na unywaji Maji yasiyo masafi kwa kaya zinazoishi katika mikoa ya Shinyanga na Ruvuma (Madama, Namtumbo, Songea, Kahama / Msalala, Shinyanga DC, MbogweWilaya), Tanzania. PoA inasimamiwa na 4Life Solutions (zamani inayojulikana kama SolarSack), iliyo na ofisi kuu Kidenmaki inaanza. Katika muktadha huu Ushauri wa Umma wa Wadau wa Mitaa utafanyika kwa wadau wote wa ndani ya nchi, walioathirika na wanaovutiwa, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali, vikundi vya wanawake, taasisi za utafiti na mashirika / watu wanaofanya kazi juu ya mada zinazohusiana na shughuli za mradi, watunga sera juu ya kitaifa na ngazi ya wilaya na pia kwa watu wa eneo, jamii na wawakilishi ambao wameathiriwa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja na mradi huo.

4LIFE Solutions (Waratibu na wasimamizi Taasisi ya PoA) inaalika watu wote wanaopenda kuhudhuria
**Ushauri wa Wadau wa Mtaa mnamo Oktoba 29th, 2021, 8:30 asubuhi hadi 13:00 jioni katika**
**Ruhuwiko Hunt Club**
**Mji wa Ruhuwiko-Songea**
**Mbinga road**
**Tel N ° ya ukumbi+255620655773 AU +255252951008**

Wadau ambao hawawezi kuhudhuria mkutano huo, wana uwezekano wa kushiriki mkondoni kupitia Zoom. Maelezo ya kuingia ni yafuatayo:

Umealikwa kwenye mkutano wa Zoom.
**Wakati: Oktoba 29, 2021 08:30 AM E.A.T (MUDA WA AFRIKA MASHARIKI)**

Jisajili mapema kwa mkutano huu ukitumia kiunga hiki:
**https://us02web.zoom.us/meeting/register/tZAsfuivqT8pG9FuSHs5itwOHbQDg7-5ZN1U**

Baada ya kujiandikisha, utapokea barua pepe ya uthibitisho iliyo na habari juu ya kujiunga na mkutano huo.

### AJENDA

- Mapokezi - Kutia saini orodha ya washiriki (8:30 asubuhi)
- Utangulizi na uwasilishaji wa Mradi (9:00 asubuhi)
- Maswali na maoni juu ya mradi huo (9:30 asubuhi)
- Kanuni za Kulinda Tathmini ya mradi (10:30 asubuhi)
- Tathmini endelevu ya mradi (11:15 am)
- Majadiliano juu ya utaratibu wa malalamiko na ufuatiliaji wa athari za maendeleo endelevu (12:15 pm)
- Fomu za tathmini na kufungwa kwa mkutano (12:30 pm)
- Maonyesho (12:45 pm)
- Chakula cha mchana (13:00 pm)

**www.4lifesolutions.com**

Ikiwa kuna maswali yoyote au ikiwa unataka maelezo zaidi na habari za mradi kabla ya mashauriano, tafadhali andika barua pepe kwaJulius Macharia, Meneja wa Kaboni kutoka 4LIFE Solutions (jkm@4lifesolutions.com) au piga simu kwa Happiness Urasa, Msimamizi wa Miradi nchini Tanzania kutoka 4Life Solutions (+255 767 007 505) Tafadhali tumia maelezo haya ya mawasiliano pia kwa kutoa maoni yako ikiwa huwezi kushiriki katika mkutano wa wadau.

216482301

# Ajinyonga hadi kufa kwa msongo wa mawazo

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MKAZI wa Kijiji cha Kasuhunga, wilayani Bunda, Majami James (57), amekufa kwa kujinyonga na kamba ya katani kwenye mti uliokuwa nyuma ya nyumba yake na kuacha ujumbe kuwa ameamua kujitoa uhai kutokana na msongo wa mawazo

Kamanda wa Polisi mkoani Mara, Longinus Tubishubwamu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana.

Alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 12 alfajiri eneo la nyumbani kwa marehemu, kijijini hapo.

James ambaye alikuwa mjasiriamali wa kibanda cha duka la vitu vidogovidogo, pia alikuwa fundi cherehani akiwa anajishughulisha na ushonaji wa nguo za aina mbalimbali kijijini hapo.

Kamanda Tubishubwamu alisema kuwa siku moja kabla ya kuchukua uamuzi huo, kulikuwa na kikao cha wanafamilia kikiwa kinamjadili kuhusu mwenendo wake wa kimaisha pamoja na wana ukoo wenzake.

"Siku moja kabla ya mwanamume huyo kuamua kujitoa uhai wake kulikuwa na kikao cha wanafamilia kikimjadili masuala mbalimbali juu ya mwenendo wake wa kimaisha," alisema kamanda Tubishubwamu.

Alisema kuwa siku iliyofuata mwili wa James ulikutwa unaning'inia juu ya mti nje kidogo ya nyumba yake.

Alisema kuwa baada ya kufanya upekuzi kwenye mfuko wa nguo yake, walikuta karatasi iliyokuwa na maandishi, 'Asisumbuliwe mtu yeyote kuhusu kifo changu, kwani nimeamua kujitoa uhai wangu mwenyewe kutokana na msongo wa mawazo'.

Kufuatia tukio hilo kamanda Tubishubwamu, aliendelea kutoa wito kwa wananchi, kumrudia Mwenyezi Mungu kwa kuacha kutenda mambo maovu, ikiwa ni pamoja na kupata ushauri nasaha kwa watu mbalimbali wakiwamo viongozi wa madhebu ya dini, wanapokutana na changamoto za kimaisha ili waweze kushauriwa vizuri.

Alisema kuwa tayari mwili wa marehemu umehifadhiwa katika chumba cha maiti katika Hospitali teule ya Halmashauri ya mji wa Bunda (CDH).

Baadhi ya wakazi wa kijiji hicho waliozungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka kijiji hapo, wamesikitishwa na uamuzi huo wa kujinyonga, kwa kuwa alikuwa mtu mpole na muda wote alikuwa akishinda ndani ya kibanda chake.



Mabinti balehe na kinamama vijana wenye umri kati ya miaka 17 hadi 24, wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wanaosoma fani ya ufundi magari wakijifunza kwa vitendo katika Chuo cha Ufundi stadi Mwaka, katika Halmashauri ya Msalala juzi, kwa ufadhili wa Shirika la FHI360 chini ya USAID na PEPFAR. Habari Uk. 7. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Watatu wanaodaiwa majambazi wauawa

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WATU watatu wanaodaiwa kuwa majambazi wa kutumia silaha waliokuwa wakijiandaa kutekeleza tukio la uhalifu katika eneo la Kwa Maiko, Kata ya Nyakitonto, Wilaya ya Kasulu, wameuawa wakati wa majibizano ya risasi na polisi.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, ACP James Manyama, alisema tukio hilo limetokea juzi majira ya saa 11 alfajiri baada ya kupata taarifa za uwapo wa wahalifu waliotega magogo kwa ajili ya kupora wananchi na wafanyabiashara wanaotoka katika eneo la Kagerankanda.

Kamanda Manyama alisema baada ya wahalifu kubaini kuwa wanafuatiliwa walianza kurusha risasi dhidi ya polisi na kikosi cha TANAPA Hifadhi ya Gombe, waliokuwa kwenye doria hiyo. Polisi walifanikiwa kuwajeruhi wahalifu hao

Kamanda Manyama alisema wahalifu wote watatu wamepoteza maisha wakati jeshi hilo likiwapeleka kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu.

Polisi pia imekamata bunduki aina ya AK47, magazine moja yenye risasi 24 na mapanga katika eneo la tukio pamoja na kubaini kuwapo na genge la wahalifu sita na zoezi la kuwatafuta wengine waliokimbia likiendelea.

Waliofariki wanakadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 35 hadi 40 na majina yao hayajatambuliwa.

"Operesheni zetu ni endelevu kama kuna watu wako maeneo yale wakitarajia kutenda uhalifu hakika tutawamaliza wote," alisema.

# Mashahidi zaidi wa Jamhuri kutoa ushahidi kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KESI ya uhujumu uchumi namba 27, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita, inatarajiwa kuendelea kunguruma leo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, ambapo mashahidi wa Jamhuri watatoa ushahidi.

Washtakiwa wengine ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Septemba 23, mwaka huu akitoa ushahidi, aliyekuwa Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Renatus Msangira (45), alidai kwamba Ole Sabaya, hakupewa kibali chochote cha maandishi kwenda kutekeleza majukumu nje ya kituo chake cha kazi.

Msangira, ambaye ni shahidi wa kwanza wa upande wa Jamhuri, alitoa madai hayo, wakati akitoa ushahidi, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia.

Alidai kiutaratibu Mkuu wa Wilaya akitaka kwenda kufanya kazi nje ya kituo chake cha kazi inatakiwa apate kibali cha maandishi kutoka kwa Mkuu wa Mkoa, lakini hilo halikufanyika.

Naye shahidi wa pili wa Jamhuri, ambaye ni Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Arusha, Kayobio Majogoro(41), alidai ofisi yake, haikuwa na taarifa za Sabaya, kuongoza kikosi maalum kwenda kufanya operesheni ya kukusanya kodi jijini Arusha.

Septemba 24, mwaka huu, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofmed Mtenga, alidai kwa mujibu wa sheria, Kamishna Mkuu wa TRA, ndiye mwenye mamlaka ya kuunda kikosi kazi maalum kwa ajili ya kukusanya na kuchunguza masuala ya kikodi.

Majogoro alidai suala na kukusanya kodi lipo chini ya mamlaka hiyo na wakuu wa wilaya hawahusiki kukusanya kodi, bali wanabaki kuwa kama wadau wa taasisi hiyo ya serikali.

Alidai vyombo vingine vya dola wakiwamo askari wanashirikiana nao kwa kuwaomba msaada kama wanakwenda kufanya operesheni maalum ya kukusanya kodi au kufanya uchunguzi.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume na Sheria ya Uhujumu Uchumi Kifungu cha 57(1) na 60(2) na linawakabili washtakiwa wote.

Ilidaiwa kwa pamoja washtakiwa hao, Januari 22, mwaka huu katika maeneo tofauti ya Jiji la Arusha, akiwa mtumishi wa serikali kwa nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, walifanya vitendo vya uhalifu kwa kujipatia fedha kiasi cha Sh. milioni 90 kwa manufaa yao.

Shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake.

Ilidaiwa Januari 22, mwaka huu, eneo la kwa Murombo jijini Arusha, Sabaya alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kumtaka Francis Mrosso, kumpatia Sh. milioni 90 kwa kumshinikiza ili asitoe taarifa za jinai za mtu huyo za madai ya ukwepaji kodi.

Shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya ruswa linamkabili Sabaya, ambapo ilidai Januari 22, mwaka huu, akiwa katika eneo la kwa Morombo jijini Arusha, alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kujipatia Sh. milioni 90, kutoka kwa Francis Mrosso, ili asitoe taarifa za jinai za mtu huyo za madai ya ukwepaji kodi.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, linamkabili Sabaya peke yake, ambapo ilidaiwa kuwa, Januari 22 mwaka huu, akiwa katika eneo la kwa Murombo, alitumia vibaya nafasi yake ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, kwa kumtisha Francis Mrosso, kumfungulia mashtaka ya kukwepa kodi na.

Shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linawakabili washtakiwa wote saba, Inadaiwa Februari 22, mwaka huu, Ole Sabaya kwa kushirikiana na wenzake, wakiwa katika eneo la kwa Murombo Jijini Arusha, walijipatia Sh.milioni 90, wakitambua kufanya hivyo ilikuwa ni zao la vitendo vya rushwa.

# Mwongozo kuhusu ukatili jinsia wazinduliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imezindua mwongozo wa sera ya nyongeza ya ushirikiano wa majukumu baina ya kada za afya kuhusu ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya watoto na ujazaji wa fomu za matibabu kutoka polisi (PF3).

Aidha, mwongozo huo utawezesha waathirika wa ukatili wa kijinsia, hasa wanawake na watoto kupata huduma bora za matibabu.

Akizindua mwongozo huo jana jijini Dodoma Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema masuala ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto yanahitaji jitihada za kila mwanajamii.

Alisema uwapo wa sera hiyo utawezesha waathirika wa ukatili wa kijinsia na watoto kupata huduma bora za matibabu kutokana na kuboreshwa kwa mfumo wa ujazaji wa fomu za PF3.

"Sera hii itawezesha pia kupatikana kwa urahisi ushahidi wa mtu aliyefanyiwa ukatili wa kijinsia hivyo kuondoa changamoto iliyopo hivi sasa ya kesi nyingi za ukatili wa kijinsia kukosa ushahidi wa kutosha," alisema.

Pia Dk. Gwajima alisema ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinalindwa na siyo kuiachia serikali pekee yake.

Alisema katika kupambana na tatizo la ukatili wa kijinsia, serikali imeandaa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto kwa lengo la kupunguza kiwango cha ukatili katika jamii kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

Alisema, mpango huo ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000, Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia wa mwaka 2005, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008, Sheria ya Makosa ya Kujamiiana – SOSPA ya 1998.

"Pamoja na uwepo wa mpango hatuwezi kufikia malengo haya kama hatutawajibika kwa pamoja katika kupiga vita suala la ukatili wa kijinsia, hivyo tunahitaji kuwa na mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika kufanikisha malengo haya," alisema.

Kadhalika, alisema bado ipo changamoto ya ushahidi wa kutosha kutopatikana hali inayochangia kesi nyingi za ukatili watuhumiwa kushinda.

# Samia, Blair wateta Dodoma



Rais Samia Suluhu, akizungumza na Waziri Mkuu Mstaafu wa Uingereza, Tony Blair Ikulu Chamwino Jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alikutana na kufanya mazungumzo na Waziri Mkuu Mstaafu wa Uingereza, Tony Blair, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Tony Blair ambaye ni Mwenyekiti Mtendaji wa Taasisi ya Mabadiliko Duniani (Tony Blair Institute for Global Change) alimshukuru na kumhakikishia Rais Samia kuwa taasisi yake inaunga mkono jitihada mbalimbali anazochukua katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania.

Alisema ili kuwa na mafanikio ya haraka katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ni muhimu kuwa na taarifa sahihi ambazo zitawezesha ufuatiliaji wa karibu wa miradi hiyo.

Kwa upande wake, Rais Samia amemshukuru Tony Blair kwa kukutana naye na kumjulisha ufuatiliaji na uratibu wa masuala yanayofanywa na taasisi yake katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini Tanzania.

Pia Rais Samia alisema kwa sasa serikali inaendelea na utekelezaji wa vipaumbele vyake kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.







# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Upangaji wa wamachinga uzingatie haki za binadamu

**MWENENDO** mzima wa ufanyaji wa shughuli za ujasiriamali wa kujitafutia riziki kupitia biashara ndogo katika maeneo mengi nchini ni changamoto.

Ni changamoto kwa kuwa shughuli hizo hazifanyiki inavyopaswa, ingawa hakuna wa kulaumiwa moja kwa moja katika hilo.

Kuna watu wanaowalaumu wafanyabiashara wadogo (wamachinga) kwamba wanafanya biashara holela bila kufuata sheria, kanuni na taratibu hususan kwenye maeneo wasiyoruhusiwa huku upande mwingine ukizilaumu mamlaka za serikali kwamba ndizo chanzo, kutokana na kutowapangia maeneo rafiki.

Wamachinga wamekuwa wakilalamikia kupelekwa katika maeneo yasiyofaa kwao, ikiwamo kutokuwa na wateja wa kuwauzia bidhaa zao wakati halmashauri zikiwaondoa kwa nguvu kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.

Kasoro kubwa ambayo tumekuwa tukiiona katika mchakato wa kuwaondoa wamachinga kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kufanyiwa biashara ni operesheni hizo kutekelezwa usiku bila wahusika (wamachinga) kuwapo.

Hali hiyo husababisha kuvunjiwa vibanda vyao, hivyo mali zao kuharibiwa na matokeo yake kuwaingiza katika hasara kubwa, ikizingatiwa kuwa wengine walizinunua bidhaa hizo kwa fedha za mikopo.

Hivyo kwa kuzingatia suala zima la haki za binadamu, tunaona njia bora ya kuwaondoa ni wanaotekeleza operesheni hizo kuwa na sura ya huruma na kutumia busara pamoja na kutanguliza suala la haki za binadamu. Kwamba operesheni zitekelezwe mchana ili walengwa waondoe mali zao.

Tunasema hivi kwa kuzingatia maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa hivi karibuni kwa wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanawapanga wamachinga badala ya kuwabugudhi. Neno kuwapanga tafsiri yake si kuwaondoa kwa mabavu bali kuwatafutia maeneo maalum rafiki na kuwaondoa walipo kwa njia zinazokubalika, ambazo haziwasababishii karaha, usumbufu na mateso.

Tunayasema haya katika kuweka msisitizo kwa halmashauri zetu katika utekelezaji wa agizo la Rais la kuwaondolea wamachinga manyanyaso na kubughudhiwa kwa kuwapanga, baada ya kusikika malalamiko mkoani Dar es Salaam.

Yametolewa malalamiko kuwa operesheni inayoendelea kutekelezwa ya kubomoa vibanda vya wafanyabiashara wadogo katika maeneo yasiyo rasmi mkoani Dar es Salaam imeleta kilio kwao, huku wakisema imewadidimiza kiuchumi na kurudisha nyuma maendeleo yao.


Wanalalamika kukumbana na kadhia hiyo baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, kuzindua mpango wa kuwapanga katika eneo la Gongo la Mboto kwa kuvunjiwa vibanda vyao, huku wengine wakidai kupoteza baadhi ya bidhaa zao. Wanalalamika kuwa kubomolewa vibanda vyao kumewarudisha nyuma kimaendeleo, kwani walikuwa wanajikimu kimaisha kupitia biashara hizo.

Hatupingani na operesheni za kuwaondoa wamachinga katika maeneo yasiyo rasmi kwa kuwa sio sehemu rafiki na ni kuvunja sheria, na kanuni na taratibu za mipango miji, isipokuwa viongozi wa mamlaka husika wasitumie mabavu bali ushawishi, busara na kuzingatia maelekezo ya Rais Samia.

Wakumbuke kwamba hao ni Watanzania kama wao na watilie maanani kwamba nchi yetu kama zingine duniani zinakabiliwa na umaskini na ukosefu wa ajira, hivyo ujasiriamali ndiyo njia pekee ya kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Haya ndiyo makundi hatarishi ya TB inayoua 70 kila siku duniani

**RIPOTI** ya Shirika la Afya Duniani (WHO), inaonyesha kuwa Tanzania inaendelea kupiga hatua katika kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa asilimia 18, hadi mwaka jana.

WHO lilitathmini nchini, kwa kushirikiana na wataalamu kutoka nje na ndani, kuona namna tulivyofikia malengo tuliyojiwekea kwenye mpango mkakati wa mwaka 2015, ikiwamo kuongeza kasi ya kuwafikia wagonjwa kwa asilimia 29 zaidi.

Ripoti hiyo iliyotolewa mwaka jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Zainab Chaula, katika kilele cha mkutano wa kupokea taarifa ya tathmini ya mpango mkakati wa tano wa mwaka (2015-2020) wa Kifua Kikuu na Ukoma.

Ni hatua nzuri zilizofikiwa, lakini itapendeza iwapo mapambano hayo yatapanuliwa kwa kumshirikisha kila mtu, huku elimu kwa umma ya kutambua dalili za TB ikipewa kipaumbele zaidi.

Kwa nini? Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa ugonjwa huo unaua watu 74 kila siku, huku makundi hatarishi yakitajwa ni ya wanaotumia dawa za kulevya, wakiwamo wanaojidunga sindano.

Dk. Saitole Laizer, anatoa taarifa hiyo kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Serikali, katika uzinduzi wa muungano wa wadau wa kupambana na kifua kikuu nchini, kwamba ugonjwa huo bado ni tishio, ingawa wengi hawajui kuwa unaua. Kimsingi, utaendelea kuua ikiwa juhudi za makusudi hazitachukuliwa haraka.

Anafafanua kwamba, katika takwimu hizo za mwaka 2018, vipimo vinaonyesha kati ya watu 133,000 wanaopimwa, 227 hukutwa na maambukizi, hivyo kuifanya Tanzania kuwa na wagonjwa 1,600 wa TB sugu, na kati yao 400 waligundulika mwaka jana pekee.

Kuisaidia katika vita hiyo, waliowahi kuugua wakatibiwa na kupona, wanaweza kuwa walimu wazuri kwa umma kuzijua dalili za TB, ili waende kupata vipimo sahihi, badala ya kuamini wamelogwa.

Watu hao watakapotumika vizuri kutoa elimu, watasaidia kuwafanya Watanzania watambue jinsi ugonjwa huo unavyoenezwa na watakuwa makini kuepuka mazingira hatarishi yanayoweza kusababisha wakaambukizwa.

Hao wanajua kuwa kuboresha usafi wa mazingira, kuishi katika nyumba zenye hewa safi na kuepuka msongamano wa watu, ni mojawapo ya njia ya kuepuka TB inayotajwa inatibika licha ya kuwa hatari, inatibika.

Pia, wanajua kwamba kupungua uzito, kutokwa na jasho jingi nyakati za usiku, kukohoa kwa muda wa wiki mbili mfululizo, ni dalili nyingine za mtu kuwa na ugonjwa huo, hivyo si vibaya wakatumika kuelimisha.

Kwa kutambua mazingira hayo hatarishi, ni wazi kila Mtanzania atajihadhari na kuchukua hatua anapohisi dalili, kutokana na ugonjwa huo unaweza kumpata mtu yeyote na kwa wakati wowote.

Hivyo, suala la elimu kwa umma likiwekewa mkazo, wale ambao wamekuwa wakiugua na kukimbilia kwa waganga wa kienyeji, nao watambue umuhimu wa njia sahihi za matibabu.

Ni namna bora inayomfanya kila mtu atambue ni elimu kwa umma, hasa kwenye maeneo ambako nyumba zimesongamana, ni mazingira yanayoweza kusababisha wakazi wa huko kupata ugonjwa huo kirahisi.

Ushauri wa kushirikisha kundi hilo katika utoaji wa elimu ninautoa, kwani siamini kama watumishi wa sekta ya afya pekee yao wanaweza kutosha kuzunguka nchi nzima kuelimisha umma, hivyo wakiongezewa na hao niliowataja, inawezekana kukawa na matokeo chanya zaidi katika kukabiliana na TB.

Ikumbukwe, wataalamu wa afya wanaitaja TB katika orodha ya magonjwa duniani, unaua watu wengi kuliko katika idadi ya juu kutoka orodha ya magonjwa hatari, inaambukiza kwa kasi, lakini inatibika.

Sababu za kifua kikuu kuua kwa kasi, zitajwa kuwa zinachangia ugonjwa huo kuua, ni watu wanaoumwa kukatisha kutumia dawa kabla ya muda waliopangiwa na hivyo kujikuta wanapoteza maisha.

## HABARI KITAIFA

# Viongozi wa dini waombwa kutoa elimu mabadiliko ya tabianchi

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewaomba viongozi wa dini kutoa elimu kuhusu athari za mabadiliko ya tabia nchi na kelele kwa afya za wananchi ili kulinda vizazi vya sasa na vijavyo.

Amesema kwa mwezi Mei hadi Septemba, mwaka huu pekee jumla ya malalamiko 85 yaliripotiwa katika Mkoa wa Dar es Salaam huku maeneo yanayoongoza kulalamikiwa yakiwa ni kumbi za starehe na burudani.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua semina ya siku moja iliyoandaliwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEC) kwa viongozi wa dini wa Mkoa wa Dar es Salaaam.

Alisema kwa kipindi hicho malalamiko kuhusu kumbi za burudani yalikuwa 65 huku yale yanayohusu nyumba za ibada yakiwa 20 na kuomba ushirikiano wa wadau wote katika kutokomeza malalamiko ya aina hiyo.

Makalla alisema katika siku za karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la mitetemo na kelele zinazotokana na shughuli mbalimbali jambo ambalo linaathiri afya za wananchi.

Alisema baadhi ya malalamiko ya wananchi yamekuwa yakitolewa dhidi ya nyumba za ibada jambo ambalo NEMC imekuwa ikisaidia kutoa elimu ili kulinda vizazi vijavyo.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema mkutano huo umekuwa wa mafanikio makubwa kwa kuwa viongozi wengi wa dini wamekiri kuwa awali hawakuwa wanafahamu sheria na wameondoka na uelewa mpana.

"Kwenye michango yao wamesema wanakwenda kuwa walimu kwa waumini wao au watu wanaowahudumia na wameitaka NEMC kuendelea kutoa elimu kwa jamii, ili wafahamu sheria ya usimamizi wa mazingira.

Alisema NEMC iliamua kuwaita viongozi wa dini kuwapa elimu hiyo baada ya kubaini kwamba wengi hawakuwa wanajua wanapozidisha sauti inakuwa kelele na kusababisha na madhara mbalimbali.

Alitaja baadhi ya athari za kelele kuwa ni madhara ya akili, msongo, hofu, maumivu ya kichwa mabadiliko ya kihisia kwenye mapenzi (importance), kuongezeka kwa migogoro ya kijamii, usumbufu wa usingizi ambayo mwisho wake husababisha shinikizo la damu.

Alisema kelele zimekuwa zikisababisha uchovu, huzuni, kupunguza uwezo wa kazi, kutokujiamini, uwezo mdogo wa kufanyakazi na kuharibu uhusiano na maelewano na watu.


**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**TENDER CANCELLATION NOTICE**

**REQUEST FOR PROPOSAL:**
**No. RFP/KAS/SUPPLY/2021/SUP/001**
FOR THE CONSTRUCTION OF NEW OFFICE BUILDINGS AT UNHCR KIGOMA

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam has cancelled this tender which was accessible in the link below.

https://drive.google.com/drive/folders/1RlhoxKP-xXoHNKguM0GwAP6MZ5 roddFV?usp=sharing

216483901



**Air Tanzania**
The Wings of Kilimanjaro

**TRAINING INSTITUTE**

**TANGAZO LA MNADA**

Wananchi wote wanatangaziwa kwamba, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) watauza kwa njia ya Mnada wa Hadhara magari .

| TAREHE | KITUO | AINA YA VIFAA |
|---|---|---|
| 16/10/2021 | Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) – J.Nyerere Int'l Airport Term 1 Admin Block. | Toyota Landcruizer 6<br>Toyota Coaster 1<br>Toyo Tractor 1<br>Toyota Hiace 1 |

**MASHARTI YA MNADA:-**

1. Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo mahali kilipo;
2. Mnunuzi atalazimika kulipa amana papohapo sichiniya asilimia ishirini natano (25%) yathamani ya Chombo/Kifaa alichonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14), kuanzia tarehe ya kifaa kunadiwa. Kushindwa kufanya hivyo kutamuondolea mnunuzi haki zote za ununuzi wa Chombo/kifaa kinachohusika na AMANA (Deposit) haitarudishwa;
3. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa sikusaba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;
4. Ruhusa ya kuangalia vyombo hivyo itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya Mnada;
5. Mnada utaanza saa nne (4:00) asubuhi.

**MKURUGENZI MKUU**
**KAMPUNI YA NDEGE TANZANIA (ATCL)**




PO Box 123456 / Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +254 20123456 / Fax +254 20123456 /email:info@airtanzania.com
website:www.airtanzania.com

216484902

# Gwajima aonya NGO ukiukwaji sheria

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameyataka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) kujiepusha na ukiukwaji wa sheria, taratibu na miongozo iliyopo.

Akifungua Mkutano wa Mwaka wa Mashirika hayo jijini hapa, Waziri Gwajima alisema baada ya mkutano huo hataraji kupokea malalamiko ya ukiukwaji wa misingi ya sheria kutoka pande zote za Serikali na Mashirika.

Gwajima alitaka kuwepo na mifumo ya kujiratibu katika kuisaidia kutatua kero kwa kushirikiana na jamii zinazowazunguka.

Aidha, Waziri Gwajima serikali iko tayari kupokea maoni na kero kupitia Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCONGO).

"Kule mnakofanya kazi kwenye mikoa na halmashauri tunatamani kuona kwenye mipango yao ya kila mwaka 'visibility' yenu ionekane kwenye mipango yao. Hatujasema mzichukue zile hela mzipeleke, huenda mkawa na utaratibu wenu lakini kwenye kazi ambazo mnatoa fedha zikaonekane pale," alisema.

Gwajima alisema lengo la serikali ni kuendelea kujenga, kuboresha na mazingira wezeshi kwa Mashirika hayo ili kufanya kazi kwa ufanisi na kuchochea maendeleo ya taifa.

Dk. Gwajima alisema serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na NGO katika kuisaidia serikali ili kuwaletea wananchi maendeleo.

"Mashirika yanakwenda hatua kwa hatua na serikali na hata maendeleo haya tuliyonayo na hapa tulipofika ni kutokana na mchango mkubwa wa mashirika haya," alisema.

Alihimiza mashirika hayo kushirikiana na watendaji kwenye maeneo yao kuhakikisha elimu ya chanjo ya corona inatolewa kwa kina, ili wananchi wajitokeze kwa hiyari kuchanja.

Awali, akiwasilisha maelezo kuhusu ofisi yake na huduma za uratibu na usajili, Msajili wa Mashirika hayo, Vickness Mayao, alisema lengo la mkutano huo ni kuimarisha ushirikiano na uhusiano wa NGO na serikali kwa kujadiliana kero zilizopo na namna ya kuzitatua kwa kuzingatia sheria na sera.

Naye Mbunge wa Viti Maalumu anayewakilisha Mashirika hayo, Neema Lugangira, aliiomba serikali kufanya mapitio ya kanuni ya fedha ya NGO ya kuwezesha kupata vibali mapema ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.



Mkazi wa Dar es Salaam akiruka maji yaliyojaa kwenye barabara ya Mtaa wa Pamba, eneo la Posta, kutokana na mvua iliyonyesha jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## TMA yawaondoa hofu wananchi kuhusu mvua

**Na Faustine Feliciane**

KUTOKANA na mvua zinazoendelea kunyesha kwenye baadhi ya maeneo nchini, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Imesema mvua hizi si za msimu na si endelevu.

Mtaalamu wa utabiri wa TMA, Rose Senyagwa, alisema mvua zinazonyesha sasa ziko nje ya msimu na ni za kawaida zinazotokana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

"Hizi mvua zinazonyesha sasa wala si endelevu ndiyo maana tunaona kuna vipindi vya muda mrefu vya jua. Mvua za msimu bado hazijaanza," alisema Senyagwa.

Alisema kuwa mvua zinazonyesha sasa ni nyepesi ingawa kwa siku ya jana zilinyesha kubwa kidogo.

" Mvua zenyewe za msimu tunazitarajia kuanza kati ya wiki ya kwanza mpaka ya tatu ya Oktoba kama ambavyo tulivyotoa utabiri. Hizi za sasa wananchi wasiwe na shaka ni za kawaida ambazo zipo nje ya msimu," alisema Senyagwa.

Katika utabiri uliotolewa mapema mwezi huu kwa mvua za vuli kwa mikoa inayopata mvua inaonyesha maeneo mengi yatakumbwa na ukame kutokana na mifumo ya hali ya hewa kuonyesha kutokuwapo kwa mvua nyingi kwa nchi.

Hali hiyo imesababisha TMA kutoa tahadhari ya ukame kwa baadhi ya mikoa, hivyo kuwataka wananchi na mamlaka husika kuchukua tahadhari kwa athari zitakazotokana na uhaba huo wa mvua.

**Mvua zenyewe za msimu tunazitarajia kuanza kati ya wiki ya kwanza mpaka ya tatu ya Oktoba kama ambavyo tulivyotoa utabiri. Hizi za sasa wananchi wasiwe na shaka ni za kawaida ambazo zipo nje ya msimu," alisema Senyagwa.**

# Kukabili ukatili kijinsia kwahitaji wanawake

**Na Happy Severine,** MASWA

SHIRIKA la Kawiye Social Development Foundation (KASODEFO), limesema jitihada za kuondoa ukatili wa kijinsia zinahitaji ushiriki wa wanawake wenyewe.

Meneja Programu wa Shirika hilo, Marius Isavika, aliyasema hayo jana wakati akifungua kikao cha kujadili mikakati ya kupambana na tatizo hilo wilayani Itilima, mkoani Simiyu. Alisema tangu mwaka 2017, shirika hilo limekuwa likitekeleza mradi huo kwa mafanikio na mwaka huu, limerudi baada ya awamu ya kwanza kumalizika Machi,mwaka huu, na kwamba umelenga kuimarisha jamii kupinga ukatili wa wanawake na watoto wa kike.

"Mradi wetu unafanyika kwa ubia wa Shirika la Foundation For Civil Society kwa ruzuku ya Sh. milioni 34.500,000 utatekelezwa kwa kipindi cha miezi sita, Agosti mwaka huu hadi Machi 31, mwakani,"alisema.

Alisema ili kupata mafanikio mazuri, taasisi imejipanga kufanya kazi na kamati za kupinga ukatili wa kijinsia za kata zijulikanazo kama kamati MTAKUWWA.

Alisema wataelekeza nguvu nyingi kwa wasichana waliopo shuleni, ili kuwajengea stadi za maisha pamoja na kuwapa elimu ya kujitambua.

"Tumepanga kuvijengea uwezo vikundi vya kina mama kutoka kata za Chinamili, Ikindilo na Mwamtani katika eneo la uraghbishi ili wawe mabalozi kwa makundi ya wanawake kupinga vitendo hivi,"alisema Isavika.

Kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia kwa sasa, Isavika alisema kuna mabadiliko makubwa ndani ya kipindi cha miaka minne iliyopita ambayo shirika limekuwa likifanya kazi kwa vipindi tofauti tofauti.

Katika kipindi cha utekelezaji, nguvu nyingi itawekwa kwenye utengenezaji wa mawakala wa mabadiliko kutoka kwa mabinti walioko shuleni pamoja na kutumia mbinu za kiraghibishi kwa wana jamii wa kawaida.

Alisema awamu hii wanategemea kupata matokeo makubwa kwa kundi lengwa sambamba na mabadiliko jamii itakayofikiwa.

HABARI KITAIFA

## Viwanda saba dawa vyajengwa mwaka 1

Na Mary Geofrey

MKURUGENZI Mkuu wa Bohari ya Dawa (MSD), Meja Jenerali Gabriel Mhidze, amesema katika kipindi cha mwaka mmoja alichoteuliwa kushika nafasi hiyo, wamefanikiwa kuanzisha viwanda saba vya kutengeneza dawa na vifaa tiba kwa gharama ya Sh. bilioni 16.

Alisema kwa kushirikiana na wataalam wa MSD wameanzisha viwanda vya kutengeneza dawa za vidoge na dawa za rangi mbili, majitiba, mipira ya mikononi (cloves), barakoa, vitakasa mikono, dawa za watoto na dawa za ngozi yakiwamo mafuta tiba kwa watu wenye ulemavu wa ngozi.

Meja Jenerali Mhidze, alieleza mafanikio ya MSD na malengo yake kwa waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam na kusema kuwa kuwapo kwa viwanda hivyo kutasaidia kupunguza gharama za dawa na vifaa tiba.

"Gharama ya kuanzisha kiwanda kimoja ni Sh. bilioni 40, lakini sisi tumefanikiwa kuanzisha miradi hii ya viwanda saba hadi hapa vilipofikia, vingine vimeanza kazi vingine bado vipo hatua za kukamilika kwa gharama ya Sh. bilioni 16," alisema Meja Jenerali Mhidze.

Alisema wameendelea na ujenzi wa viwanda na kuvifanyia maboresho vilivyopo ili kuongeza kasi ya upatikaji wa dawa na vifaa tiba nchini .

"Wakati naingia hapa MSD Mei mwaka jana, hali ilikuwa siyo nzuri, kwani tuliingia katika balaa la janga la UVIKO-19, barakoa ilikuwa ikiuzwa kwa bei ya juu, vitakasa mikoni navyo hali ilikuwa hivyo hivyo.

"Hata usambazaji wa dawa nao haukuwa mzuri, na sababu kubwa niliambiwa ni kutokana na UVIKO-19, niliwaita wataalamu tulionao hapa MSD na tukakusanya mawazo kupitia maandiko, kisha tukawawezesha (wataalamu) ili waanze kuanza kuanzisha viwanda," alisema.

Alisema kutokana na umuhimu wake, MSD ilianza kufanyia kazi andiko la kutengeneza barakoa na baadae, vitakasa mikono ili kukabiliana na maambukizi hayo.

"Kabla ya hapo barakoa tulikuwa tunaagiza kutoka Afrika Kusini ambako nako zilikuwa zikiingizwa kutoka China. Baadae MSD iligeukia utengenezaji wa dawa, tulianza na dawa moja na sasa tumefikia dawa 10," alisema Meja Jenerali Mhidze.

Kuhusu kiwanda cha kutengeneza mipira ya mikono kilichopo Idofya, Makambako mkoani Njombe, alisema kinatarajia kuanza kufanya kazi Novemba, mwaka huu.

Alisema kati ya viwanda hivyo, pia wataanzisha cha kutengeneza dawa za ngozi 'Cream', mafuta ya watu wenye ulemavu wa ngozi, dawa za kusafishia meno.

Aidha, alisema wamenunua mashine za kutoa tiba mbalimbali ikiwamo ya kusafisha damu kwa wagonjwa wa Figo.

Alieleza kuwa waliona kuna changamoto ya gharama za kununua mashine tiba na MSD ilikwenda kuzungumza na watengenezaji wa vifaatiba hususan mashine muhimu zinazohitajika kwa wingi katika utoaji huduma ili wazinunue kwa gharama nafuu na kuzisambaza katika vituo vya afya nchini.

# Halmashauri Buchosa sasa kuhamishiwa Mkoa wa Geita

Na Richard Makore,

MWANZA

KIKAO cha Kamati ya Ushauri mkoani Mwanza (RCC) kimeridhia kuhamishwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa iliyokuwa mkoani humo kwenda mkoani Geita.

Kikao hicho kilichofanyika jana jijini Mwanza na kufikia uamuzi huo kiliongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel.

Viongozi mbalimbali wakiwamo wabunge, wenyeviti wa halmashauri, wakurugenzi, mameya pamoja na wakuu wa wilaya zote za Mkoa wa Mwanza walishiriki katika kikao hicho.

Akizungumza katika kikao hicho, Gabriel alisema Buchosa sasa imehama rasmi kutoka mkoani kwake na kwenda mkoani Geita.

Akizungumza katika kikao hicho, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, Eric Shigongo (CCM), aliishukuru serikali kwa kufanya uamuzi huo na kuunga mkono.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni serikali kuifanya Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa iwe wilaya kamili.

Alisema Buchosa imekuwa halmashauri kwa kipindi kirefu na kwa sasa umefika muda wa kuifanya wilaya kamili ili kusaidia wananchi wake kupata maendeleo.

Wakati Buchosa ikihamishwa mkoani Mwanza, baadhi ya maeneo mkoani Geita yanatarajiwa kumegwa ili kuunda mkoa mpya wa Chato.

Mchakato wa kupata mkoa mpya wa Chato umeanza na vikao mbalimbali vilivyoshirikisha viongozi wakiwamo madiwani, wabunge, wakuu wa wilaya, wakurugenzi mkuu wa mkoa vimeshafanyika.

Wakati wa vikao hivyo vya kujadili namna ya kugawa maeneo ya Mkoa wa Geita kwenda Chato, baadhi ya viongozi walilalamikia kuhusu mipaka inavyopita, lakini baada ya majadiliano ya kina walikubaliana.



Naibu Meya wa Jiji la Tanga, Joseph Colyvas (kulia), akiwa ameshika ramani ya kidigitali yenye taarifa za kijiografia kwenye kata zao akiwa na madiwani wenzake, waliokabidhiwa kwenye mradi wa Livinglab unaoendeshwa na Tanzania Data Lab, Chuo Kikuu Ardhi (ARU) na Jiji hilo na kufadhiliwa na Foundation Botnar ya Uswisi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# ACT yaahidi ushindi ubunge Konde

Na Suleiman Rashid Omar,

PEMBA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimewahakikishia wanachama wake kisiwani Pemba kuwa mgombea wake atashinda katika uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Konde unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT-Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu, amewataka wananchi wa Jimbo la Konde kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi Oktoba 9, mwaka huu kwa ajili ya kupiga kura wakiwa wanajiamini wanayemtaka ataibuka mshindi.

Jussa aliyaeleza hayo huko Msuka katika kiwanja cha Okapi, Wilaya ya Micheweni wakati wa uzinduzi wa kampeni za mgombea wa chama hicho.

Aliwaambia wasiwe na woga bali wajitokeze kwa wingi kumchagua mgombea wa ACT-Wazalendo, Muhammed Said Issa, ili awawakilishe katika Bunge kwa ajili ya kupaza sauti zao.

" Tumchagueni Muhammed ili awe sauti ya watu wa Konde na Wazanzibar kwa ujumla akasimamie maslahi yetu na vizazi vyetu," alieleza Jussa.

Alisema wasiwe tayari kupokea ulaghai wa vyama vingine wakijidai kuleta maendeleo na kudai hawana wanaloweza kuwaletea isipokuwa vurugu na ahadi zisizotekelezeka.

"Chama pekee kinachoweza kuleta maendeleo ni ACT-Wazalendo kwani viongozi wake wana uthubutu wa kudai chochote chenye maslahi ya Zanzibar," alisema Jussa.

"Tulikuwa tukimsikia Mbunge wetu ambaye ni marehemu (Khatib Said), alivyokuwa akiitetea Zanzibar... kwa hiyo tumchagueni Muhammed ili akaendeleze pale alipopaacha marehemu," alisema zaidi Jussa.

Alivitaka vijana wasiwe wenye kukata tamaa katika kutafuta mabadiliko ya Zanzibar kutokana na vitimbi vinavyofanywa na baadhi ya watu aliowataja kuwa hawaitakii mema Zanzibar.

"Vijana tukikata tamaa tutakuwa wasaliti kwa kazi kubwa ambayo wazee wetu wameifanya kwa maslahi ya nchi yetu," alieleza Jussa ambaye alikuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe.

Alisema hana hofu na wapigakura kwani wakazi wa Pemba hawajawahi kuipigia kura CCM na kuitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuendesha uchaguzi huo kwa misingi ya haki na huru.

Alidai katika chaguzi uliopita uliosababisha aliyetangazwa kuwa mshindi baadaye kujiuzulu, NEC kwa kushirikiana na kile alichodai watu ambao hawana nia njema na Zanzibar, waliuingilia uchaguzi na kuuvuruga.

"Ninawaambia NEC tunaingia kwenye uchaguzi na tutalinda ushindi wetu na hatuko tayari kuona tunaonewa," alisema Jussa.

Kaimu Katibu Mkuu ambaye ni Katibu wa Habari na Uenezi wa chama hicho, Salim Biman, aliwataka wananchi wa Konde waende kwenye vituo, huku wakijiamini kuwa mgombea wao atashinda na atatangazwa, na kuonya kuwa yeyote atakayehujumu uchaguzi chama kitapambana naye.

Naye mgombea wa ACT-Wazalendo, Muhammed Said Issa, alisema yuko tayari kuwa mbunge wa watu wa Konde ili aweze kuwasemea katika chombo hicho cha kutunga sheria.

# Kiwanda cha kutengeneza vifaa tiba chazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Mony Industries imezindua kiwanda cha kutengeneza vifaa tiba kilichopo Kigamboni Dar es Salaam, kuunga mkono juhudi za serikali katika kurahisisha upatikanaji wa vifaa tiba nchini

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa Mony Industries, Violet Mordichai, alielezea ubora wa bidhaa zinazotokana na kiwanda hicho zinazofanya kiwanda hicho kuwa na uwezo wa kuhimili ushindani wa ndani na nje ya nchi.

Alisema: "Mony Industries imeweka kipaumbele katika utendaji unaozingatia weledi na sheria kwa ajili ya kuhakikisha kunakuwa na uzalishaji wa vifaa tiba vyenye ubora kama ilivyoelekezwa na mamlaka ya vifaa tiba - (TMDA). Kiwanda chetu ni mojawapo ya viwanda vichache sana katika ukanda wa Afrika Mashariki vyenye kutumia teknolojia ya viwango vya juu katika kuzalisha bidhaa zilizo bora."

Alisema wana mashine 7 za kisasa zenye uwezo wa kuzalisha barakoa 100 kwa dakika 1, huku kikiwa na uwezo wa kuzalisha barakoa za hospitalini, viwandani na za umma kwa ujumla.

Alisema hivi karibuni kitaanza kutengeneza glavu, hivyo kuweza kuhimili soko la ndani na la kimataifa ukiwa ni mpango wa hivi karibuni.

"Tukiwa kama wadau muhimu katika kuboresha sekta ya afya nchini, uzinduzi wa kiwanda hicho ni sehemu ya hatua ya kuunga mkono kwa vitendo juhudi za dhati za Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuongeza viwanda nchini kwetu, kuongeza ajira na vilevile kurahisisha upatikanaji wa vifaa tiba ili kufikia lengo la afya kwa wote sambamba na kujikinga na magonjwa yanayoambukiza kama vile COVID 19," Anaongeza Violet.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk Dorothy Gwajima, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo, alikipongeza kiwanda hicho kwa hatua muhimu ambazo wamechukua za kuwa sehemu ya kuboresha afya nchini, huku akiwahakikishia ushirikiano kutoka kwa serikali katika kuunga mkono juhudi hizo.

"Napenda kuwapongeza sana Bodi ya Mony Industries kwa uzinduzi huu wa maendeleo, vilevile nipende kuwajulisha kuwa serikali ipo katika kuunga mkono juhudi hizi kwani imeweka kipaumbele katika sekta ya afya hususan kuboresha na kusimamia kwa ufanisi utoaji wa huduma ya afya kwa kila Mtanzania kwa kuzingatia kuwa Taifa lenye afya ni kigezo muhimu katika kuhuisha uchumi wa viwanda na pia kurahisisha ufikiwaji wa Bima ya Afya kwa wote."

Gwajima alitoa wito kwa wanachi kuzingatia umuhimu wa afya zao binafsi kwani takwimu zinaonyesha kuwa magonjwa yasiyoambukiza yanachangia asilimia 27 ya vifo vyote vinavyotokea nchini.

"Kwa mantiki hiyo, mbali na kupoteza nguvu kazi ya taifa, kuna gharama kubwa ambazo hutumika kwa matibabu kwa magonjwa ambayo yangeweza kuyepukika kwa kula vyakula bora kwa usahihi pamoja na kufanya mazoezi na kujiepusha kwa kutumia vifaa stahili," aliongeza Waziri Gwajima.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (kulia), akipewa maelezo katika kiwanda cha Mony Industries, kinachotengeneza barakoa, wakati wa uzinduzi wa kiwanda hicho, Kigamboni Uvumba Dar es Salaam juzi. **PICHA:MPIGA PICHA WETU**

# Mhagama: Wataalamu OSHA washirikishwe sehemu zote za kazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amesema ni muhimu sehemu mbalimbali za kazi zinazoanzishwa ikiwamo migodi kuwahusisha wataalamu wa usalama na afya katika ujenzi wa awali wa miundombinu.

Lengo ni kupata ushauri utakaowawezesha kujenga miundombinu inayozingatia viwango vya usalama na afya mahali pa kazi, hivyo kuepuka kuweka miundombinu ambayo ipo kinyume na sheria na kanuni za usalama na afya mahali pa kazi.

Alisema hayo jana wilayani Ikungi mkoani Singida wakati wa ziara katika Mgodi wa dhahabu wa Shanta kwa lengo kukagua usimikaji wa mifumo ya usalama na afya katika hatua za awali za maandalizi ya uchimbaji madini.

"Kwetu sisi na wenzangu wa OSHA tutakachojitahidi ni kuendelea kuwapa elimu ya kutosha kuhusu masuala ya usalama na afya mahali pa kazi ili mbobee kwenye eneo hilo kusudi muondoshe migogoro katika eneo lenu la kazi na ndio maana ninaomba muwaruhusu hapa wawe na tawi la wafanyakazi.

Lakini tutawasaidia pia kukagua na kuangalia mifumo yenu ya usalama na afya kama itaweza kulinda afya za wafanyakazi hususan pale mtakapoanza rasmi uzalishaji kwani tunatambua kwamba shughuli hizi za uchimbaji madini huambatana na vihatarishi vingi vya usalama na afya ambavyo vinahitaji mifumo madhubuti ya kukabiliana navyo," alisema Mhagama.

Mkurugenzi wa Usalama na Afya wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Mhandisi Alexander Ngata, alitoa wito kwa kampuni kubwa ambazo zinafanya kazi na kampuni saidizi (sub-contractors) kuhakikisha kwamba zinazingatia sheria na kanuni za usalama na afya mahali pa kazi.

Awali akiwasilisha taarifa yake kuhusu hali ya usalama na afya katika mgodi huo mbele ya Waziri, Ngata alieleza kwamba kampuni hiyo imekuwa ikijitahidi kutekeleza matakwa yote ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi kama ambavyo wamekuwa wakielekezwa na wataalam kutoka OSHA.

Kaimu Meneja wa Kanda ya Kati inayojumuisha mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma, Venance Buliga, alisema wamekuwa wakishirikiana ipasavyo na uongozi wa mgodi huo katika hatua mbalimbali za ujenzi wa miundombinu ya uchimbaji madini katika mgodi huo ambapo wamekuwa wakifanya ukaguzi na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu namna bora ya kujenga miundombinu inayozingatia afya na usalama wa wafanyakazi.

# GGML yatoa mil. 800/- za kukarabati hospitali rufani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), imetoa kiasi cha Sh. milioni 800 kukarabati Hospitali ya Rufani Geita.

Pia imesaidia uchunguzi wa bure wa matibabu kwa watu wa Geita kwa siku tatu kuanzia Septemba 27, 2021 hadi Septemba 29, 2021.

Rais wa MAT, Dk. Shadrack Mwaibambe, alisema chama chake kina utamaduni wa kutoa huduma za afya bure kwa jamii kabla ya mkutano wao wa kila mwaka.

"Kwa kawaida MAT huwa na mizunguko tofauti katika mikoa yote inayotoa huduma za matibabu bure kwa jamii. Hii ni mara yangu ya kwanza kuja katika mji wa Geita na kupata vifaa vya kisasa vya matibabu ambavyo vilitolewa kama msaada kutoka GGML kwenda kwa Hospitali ya Rufani ya Geita. Msaada huu umetusaidia sana katika uchunguzi wa awali wa wagonjwa wetu.

"Wakazi wa Geita wanapaswa kujivunia uwekezaji huu wa GGML katika hospitali hii kwani vifaa vingi vinavyopatikana hapa pia vinapatikana katika hospitali kuu kama Bugando na Muhimbili. Mchango wa GGML kwa vifaa hivi vya kisasa unapaswa kupongezwa, " alisema.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa katika Hospitali ya Rufaa ya Geita, Dk. Michael Mashallah, alisema msaada wa GGML na wadau wengine waliohusika katika mradi huo utainufaisha vilivyo jamii ya wanaGeita.

"Huu ni msaada ambao umma wa aina yoyote ungependa kupata kwa sababu upatikanaji wa huduma za afya ni muhimu sana kwa sababu inaweza kuokoa maisha.

"Nawashukuru wadau wote kwa msaada wao, haswa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, GGML, MAT, AMREF, CORDET, NELICO, Fhi360, MNH, BMC, ORCI, JKI, TANCDA, Maria Stope, MDH na SHDEPHA, "alisema Dk. Mashallah.

Makamu wa Rais wa GGML, Simon Shayo, alisema kama raia na mshirika wa maendeleo, GGML imejitolea kushirikiana na serikali kuhakikisha huduma za afya zinazopatikana katika mkoa wa Geita.

Alisema kuwa GGML imetoa Sh. milioni 800 kwa Hospitali ya Rufani ya Geita kwa lengo la kuhudumia zaidi ya wakazi milioni 1.7 wanaoishi katika mkoa huo.

"GGML imekarabati majengo mbalimbali ya Hospitali ya Mkoa ya Geita, ambayo yalijengwa mwaka 1957. Pia imewapa vifaa vya matibabu vinavyoiwezesha hospitali kutoa huduma za uchunguzi wa moyo na meno.

"Msaada huu utahakikisha wana Geita wanaanza kupata huduma za matibabu ya kibingwa kama zile zilizokuwa zinatolewa kule kwenye Hospitali ya Muhimbili Taasisi ya Mifupa (Moi) jijini Dar es Salaam.

"Msaada huo umejumuisha ununuzi wa mashine ya ECG, jenereta ya dharura ya vifaa vya meno na ujenzi wa majengo ya kisasa ya dharura na kwa watoto wanaozaliwa kabla ya muda yaani njiti," alisema.

Alisema mkoa wa Geita unakua haraka na ndoto ya GGML ni kujenga vituo vya afya vya kisasa ndani jamii inayowazunguka.

"GGML imetekeleza miradi kadhaa ya afya hasa ujenzi wa zahanati huko Nyamalembo, Nyakahongola, Kasota na Kakubiro ambazo kila moja iligharimu zaidi ya Sh. milioni 260.

"Mwaka wa 2019, GGML pia ilitoa vifaa vya matibabu kwa vituo vya afya vyenye thamani ya Sh. milioni 142 kusaidia zahanati ya Katoro na Bukoli huko Geita. Katika mwaka huo huo, GGML pia ilitoa darubini mbili za kisasa zenye thamani ya Sh. milioni 13 kwa Mkuu wa Mkoa wa Geita.

# ama


**ALHAMISI SEPTEMBA 30, 2021**

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Unatumia tumbaku? Zijue sumu zake zinavyojificha mwilini na kukumaliza**



Ukurasa 12

**Magonjwa yasiyoambukiza yalivyo hatari kwa binadamu**

# Atembea Kigoma hadi K'njaro kampeni ya chanjo UVIKO 19

•Mwanariadha aliyepatiwa cheti na wizara




Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto Prof. Abel Makubi, alipomkabidhi tuzo mwanariadha Michael Nondo, aliyetembea kutoka kwao Kigoma, hadi mkoani Kilimajaro, kuhamasisha chanjo ya UVIKO 19 kitaifa. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

**Na Yasmine Protace**

ELIMU inatajwa kuwa mkombozi mkuu wa kila jambo ndani au baina ya jami. Huko nyuma Hayati Julius Nyerere, Rais wa kwanza nchini alishatamka kuwa, "elimu ni ufunguo wa maisha."

Ni nadharia ambayo wanazuoni wa fani hiyo wanaitafasiri kuwa inabeba mantiki "uelewa, ujuzi na maarifa kuhusu jambo fulani," nadharia ambayo Rais Samia Suluhu Hassan, anapenda kuisisitiza katika mtaji wake wa kudhibiti janga la maradhi ya UVIKO 19.

Jumatatu wiki hii, Rais Samia kwenye ufunguzi wa Mkutano wa Jumuiya ya Tawala za Mikoa Tanzania (ALAT), amesisitiza mbinu izame zaidi katika elimu na watu wajitokeze kuchanja katika vituo maalum vilivyoandaliwa.

Mkuu huyo wa nchi juzi alijitokeza tena kusisitiza hoja ya elimu zaidi ya umma kuchanja dhidi ya maradhi UVIKO 19, alipofungua mkutano mkubwa wa Kanisa la Anglikana nchini, jijini Dodoma, ili kuukabili UVIKO 19, ingawaje anakiri kwamba kuchanja ni shauri la hiyari.

Katika jozi ya hoja yake, Rais Samia anaambatanisha na falsafa ya watu kuhamasishwa kupata chanjo.

Msingi wa uhamasishaji huo, kama yalivyo mambo na matukio mengine, yanaendana na magumu, hali kadhalika mafanikio.

Hivyo, kutokana na kuingia ugonjwa wa UVIKO 19 katika jamii ya Kitanzania, serikali na wadau mbalimbali wamekuwa wakitoa elimu ya jinsi ya kujikinga na maradhi hayo.

Ni hivi karibuni, serikali kupitia Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia mbinu hizo anazosisitiza Rais Samia, imefikia hatua ya kumtambua mwanariadha, Michael Nondo, mkazi wa Kigoma, kupitia nyendo hizo.

Kwa vipi? Ni pale Mwanariadha Nondo, aliyejitolea kutembea kutoka mkoani Kigoma mpaka Kilimanjaro, kuhamasisha elimu dhidi ya janga hilo la kimataifa, UVIKO 19.

Ni namna ameamua kuielimsha umma, pale anapowahamasisha wananchi waelewe kwa kina kuhusu uwapo wa ugonjwa wa Uviko 19 na kushiriki chanjo dhidi yake.

Katibu Mkuu Wizara ya ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto Prof. Abel Makubi, ameueleza umma kupitia vyombo vya habari, akimwakilisha Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima jijini Dodoma, kuhusu suala hilo, akiwa na ufafanuzi wake.

"Kama serikali, tunatambua juhudi zinazofanywa na wadau mbalimbali katika mapambano haya ya corona, lakini kwa leo kama wizara niseme, tumemtambua ndugu Michael Nondo," anatamka Prof. Abel Makubi, huku akimsifu:

"Aliyeonyesha ujasiri na uzalendo wa kutembea kutoka mkoani Kigoma mpaka mkoani Kilimanjaro, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi zinazoendelea nchini kote."

Kwa kutambua mchango huo, Katibu Mkuu amemkabidhi cheti na kumpa hadhi ya ukamanda wa kuhamasisha wananchi kupata chanjo, ikiwa ni sehemu ya kuthamini mchango na uzalendo wake katika kampeni hiyo ya uchanjaji, ambayo inasisitizwa na rais.

Mwanariadha huyo kwa upande wake, anataja sababu kuu iliyomsukuma kufanya hivyo ni imani yake kwa serikali yote, pia sekta ya afya, katika mapambano dhidi ya UVIKO 19.

Hii ni mara ya pili kwa mwanariadha Nondo kufanya safari ya namna hiyo ya awali, ilikuwa Juni mwaka huu, akiwa na ufafanuzi:

"Mara ya kwanza kufanya safari hii nilikuwa nikifanya usiku, lakini hivi sasa nimeamua kufanya mchana ili kila mmoja anione. Ninawashukuru sana serikali, husussan ngazi za serikali za mitaa nilipoweza kupita.

"Walinipa sehemu za kulala na kunikutanisha na wananchi, kunitambulisha na kuongea nao kwa lengo la kutoa elimu juu ya ugonjwa huu."

Anatoa wito kwa vijana, watu wa umri wa makamo na wazee, wajitokeze kupata chanjo hizo muhimu na za hiari, akitoa wasifu wake kwamba, hazina madhara na anaushauri umma usisikilize tetesi zisizokuwa za kweli na zenye lengo la kupotosha.

Mwanariadha Nondo anahitimisha hoja yake kwa kuwataka Watanzania kufahamu, wao ni hazina inayotajiwa na taifa, hivyo wajitokeze kwenye huduma ya chanjo ya kudhibiti UVIKO 19.

AFYA

# Magonjwa yasiyoambukiza yalivyo hatari kwa binadamu

Na Mwandishi Wetu

"UKOSEFU wa mazoezi ya kutosha ya mwili ni moja ya mambo hatarishi yanayosababisha vifo duniani. Zaidi ya asilimia 65 ya magonjwa yasiyoambukiza hutokea katika umri chini ya miaka 40 kama vile ugonjwa wa moyo, shinikizo la damu, kisukari na saratani.

Dakika tatu hadi nne za mazoezi laini ya viungo kama vile kutembea au kujinyoosha hulainisha misuli na kurahisisha mzunguko wa damu.

Mazoezi ya mwili wakati wa kazi huongeza ufanisi. Mazoezi ya mwili mara kwa mara katika maisha huwawezesha watu kuishi maisha marefu na mazuri zaidi."

Ni ujumbe wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Idara ya Kinga, Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, unaohamasisha watu kuangalia afya zao mara kwa mara kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Mtu anaweza kuwa na magonjwa yasiyoambukiza kwa miaka kadhaa bila dalili zozote, lakini mwili ukaendelea kuathirika.

Kwa mfano anaweza kuishi miaka mingi na shinikizo kubwa la damu bila dalili zozote hadi pale anapopata kiharusi, moyo unaposhindwa kufanya kazi au figo zinapokuwa zimeharibika.

Ugonjwa wa kisukari unaweza usiwe na dalili hadi pale macho, figo, moyo au mishipa ya damu au fahamu inapokuwa imeharibika vibaya. Hii ni kwa mujibu wa Chama cha Kupambana na Magonjwa yasiyoambukiza (TANCDA).

Mwenyekiti wa TANCDA, Profesa Andrew Swai, anatahadharisha kuwa kila mwaka watu milioni 15 wanakufa duniani, kutokana na magonjwa ya moyo, shiniko la damu la juu, figo, sukari na kiharusi.

Anasema nchini Tanzania, watu wanakufa wengi kutokana na magonjwa hayo, kwa sababu hawana uwezo wa kumudu gharama za matibabu yake.

Lakini njia rahisi ya kuyakabili ni mtindo wa maisha ya kila siku wa kupambana na magonjwa hayo kwa kula vyakula vyenye makundi yote matano na kufanya mazoezi.

Inakadiriwa kuwa magonjwa hayo nchini Tanzania yanasababisha asilimia 27 ya vifo vyote. Utafiti wa mwaka 2012 ulionyesha kuwa kwa kila watu 100 wenye miaka 25 na kuendelea, tisa wana kisukari, 26 wana shinikizo la damu, 25 wana mafuta yaliyozidi kwenye damu na 34 wana uzito uliozidi.

Utafiti wa miaka 1986/1987 ulionyesha kuwa mtu mmoja kwa kila 100 alikuwa na kisukari na watu watano kwa kila 100 walikuwa na shinikizo la damu.



Mtu mwenye kitambi akipatiwa huduma ya kitabibu.

**KUCHUNGUZWA MAGONJWA**

Profesa Swai anasema, ili mtu kugundua mapema kama ana magonjwa yasiyoambukizwa, anashauriwa kuchunguzwa magonjwa haya:

Kisukari: Achunguzwe kila mwaka baada ya kutimiza miaka 45. Kwa wanawake, katika kipindi cha pili wakati wa ujauzito.

Shinikizo la damu: Kila mwaka baada ya kutimiza miaka 40, kila anapohudhuria kituo cha kutoa huduma za afya na kwa wanawake, kila hudhurio la kliniki za ujauzito.

Mafuta kwenye damu: Kila miaka mitano baada ya kutimiza miaka 40.

Macho: Watoto; kila mwaka hadi miaka umri wa miaka 15, watu wazima; kila mwaka baada ya umri wa miaka 40 na kila anapohitaji leseni ya udereva.

Saratani ya matiti: Kujichunguza mwenyewe matiti kila mwezi baada ya miaka 18, kuchunguzwa na mhudumu wa afya kila mwaka baada ya miaka 40.

Saratani ya shingo la kizazi: Mara moja kila miaka miwili kuanzia umri wa miaka 20 -39 na mara moja kila mwaka baada ya miaka 40.

Ugonjwa wa selimundu: Watoto wakati wa kuanza na kumaliza shule ya msingi na watu wazima ni mwaka wa mwisho wa sekondari.

**SABABU ZA KUONGEZEKA**

Mabadiliko ya mtindo wa maisha, kama vile kutofanya mazoezi, kukaa sehemu moja kwa muda mrefu na kula vyakula vya ovyo, huchangia magonjwa hayo kuongezeka.

Mtaalamu wa mazoezi kutoka TANCDA, Waziri Ndonde, anasema ni muhimu watu kuacha kubweteka na kuushughulisha mwili kwa kufanya kazi, michezo na mazoezi.

Anasema mtu anapofanya mambo hayo mara kwa mara yanakufanya uwe na utimilifu wa mwili na kuwa na uwiano.

Ndonde Anadems, kufanya mazoezi kunaufanya mwili kuwa na ukakamavu na afya iliyo imara na kushauri kila siku mtu ajitahidi kufanya mazoezi angalau kwa dakika 15 au nusu saa.

Anasema kuwa tabia ya kutopendelea kufanya mazoezi ina athari kubwa kwa sababu inachukua nafasi ya nne ya vifo vinavyotokea duniani.

**MTINDO BORA WA MAISHA**

Ulaji unaofaa ni pamoja na kula chakula mchanganyiko, chenye virutubishi vyote kwa uwiano unaotakiwa, cha kutosha kwa mahitaji ya mwili kwa ajili ya makuzi na maendeleo yake na kuwa na uzito wa kawaida kulingana na umri na urefu.

Muuguzi Mwandamizi, Elizabeth Licoco, anaeleza mambo ya kuzingatia kwenye ulaji chakula kuepuka magonjwa yasiyoambukiza kuwa ni kutokula mafuta mengi, kula matunda na mboga kwa wingi ambayo yanaasili ya nyuzinyuzi (makapi-mlo) na kusaidia katika usagaji wa chakula tumboni.

Anashauri ulaji chumvi usizidi gramu tano (kijiko kimoja kidogo cha chai) kwa mtu mmoja kwa siku na sukari isizidi vijiko vitano vidogo vya chai kwa siku.

Anataja makundi matano ya vyakula yanayotakiwa katika mlo kuwa ni nafaka, matunda, mboga, jamii ya mikunde na mafuta.

Pia anasema ulaji wa vyakula halisi husaidia upatikanaji sawa wa sukari mwilini, kwa kuhifadhi na kumeng'enya pole pole chakula tumboni. Sukari ikizidi mwilini hujaribu mishipa ya damu na fahamu, macho, figo na kongosho.

Ulaji bora kwa makundi: Anasema ulaji bora unatakiwa kuzingatia mahitaji ya mwili kutiana na jinsi, umri, mzunguko wa maisha, kazi/shughuli na hali ya afya.



Sehemu ya mahitaji yaliyoandaliwa kwa mlo kamili. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

KUTOKA KAGERA

# Aliyepata mimba kidato cha 4 asimulia mgogoro wa wazazi ulivyomnasisha

## • Mkoa, penye dini, NGO wamuunga 'imeenea hiyo'
## • Afunguka: Mama hohehahe, pia 'haziivi' na baba

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**




Wanafunzi wa mkoani Kagera wakiingia katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, katika moja ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, iliyotumika kupinga mimba za utotoni. **PICHA: MTANDAO**

MIGOGORO ya familia na wazazi na kushindwa kuzungumza na watoto wao matatizo yanayowakabili, inatajwa kuchangia ongezeko la mabinti kubeba mimba wakiwa shule, ikiwamo mkoani Kagera.

Sasa imefikia hatua imaumiza vichwa kuanzia serikalini Mkoa wa Kagera, asasi binafsi hadi na nyumba za imani.

**MAKANISANI?**

Naomi Kanyonyi, Mratibu wa Kitengo cha Kusuluhisha Migogoro na Kutetea Haki za Binadamu katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, anasema shida iliyopo ni wazazi wanakosa muda wa kusikiliza magumu ya mabinti zao.

Anatumia uzoefu wa wadhifa wake kuainisha migogoro ya ndoa kwamba inaongoza, mahsusi kundi la ndoa zenye umri chini ya miaka mitano ikilinganishwa na mingine, wakifuatiliwa na wastaafu waliokwishapata mafao.

Naomi anasema mwaka jana walipokea migogoro 797, kati yake 351 ni ya ndoa; ikifuatiwa na 200 ya ardhi; ukatili majumbani 136; urithi 70; na 28 uchawi na ushirikina.

Kanyonyi, anasema ukatili majumbani unwanagukia zaidi kinamama na watoto wao, kukiwapo imbi la wanawake waliotelekezewa familia wanaozitunza.

Mchungaji Hosseah Baraseka, Mratibu wa Vijana katika Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Lweru, anaeleza kwa mfano, binti anaweza kukutana na shida akiwa shuleni na anapojaribu kumwendea mzazi kumweleza, baadhi ya wazazi hukataa.

"Likitokea hilo mtoto anajihisi kama mtu ambaye hathaminiki katika familia na kumsababishia kuwa na mawazo tofauti, anajikuta akiingia katika vishawishi ambavyo husababisha kubeba ujauzito na kupoteza ndoto zake, anasema Mchungaji Baraseka.

Baraseka, anayeratibu shule ya Jumapili kanisani, anasema wanawahudumia vijana awaonajihisi wana shida katika jamii zao.

Anasema pamoja na wao kanisa kutounga mkono mimba za mabinti shuleni, lakini wana hoja mtoto akishakosea pia sio vema kumtelekeza, bali kumtafutia namna abadilike.

Mchungaji Baraseka anasema, kuna vijana wanaoishi maisha kinyume na ndoto zao, hivyo wanawaomba viongozi wa dini wasimame kuihubiria jamii namna ya kuwarejesha katika misingi ya dini.

Anasema baadhi ya watoto wanaobeba ujauzito kutokana na wanayoyaona katika mitandao iliyopo katika sayansi na teknolojia, kati yao wapo wanaomiliki 'simu janja' wakiwa masomoni au tabia ya baadhi ya wazazi kuwaachia watoto simu hizo.

Mchungaji huyo anasema kupitia mitandao ya kijamii watoto wanaonana na kudadisi yanayowazidi uwezo, hata kuangukia katika vishawishi.

"Utakuta kuna mtoto anapata rafiki yake wa kike au wa kiume kupitia 'facebook'. Njia hiyo sio salama kwake na Anglikana tumekuwa tukiwaeleza vijana kuhusu faida na hasara za utandawazi, ili kupunguza madhara," anasisitiza, akiongeza ufafanuzi:

"Mfano mtoto akiwa shuleni kutokana na kipato cha wazazi kutofautiana anaona wenzake wana vitu ambavyo hawezi kuvipata katika familia yake, matokeo yake anajiingiza katika mahusiano akiwa mdogo na hatimaye kupata mimba." anasema.

**KUTOKA SERIKALINI**

Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Evath Tilwetwa, anakiri wingi wa mikasa ya mimba, akirejea kikao robo ya tatu ya mwaka katika halmashauri, walipokea mikasa ya mimba 32 na watuhumiwa 17 wanatafutwa, 11 wamekamatwa na kesi tatu ziko mahakamani, huku moja imeshatolewa hukumu.

Anasema kuwa kesi hizo za mimba zipo katika shule zote za msingi na sekondari, akitaja takwimu mwaka 2019 ilikuwa na mikasa 29 kutoka shule za msingi saba na za wanafunzi wa shule za sekondari 22.

Hata hivyo, anakiri mimba zinapungua kutokana na jitihada zinazofanyika, akitoa mfano mwaka jana ilikuwa na mikasa 23 ya mimba, shule za msingi watano na sekondari 18.

"Mbali na kuunda kamati ya kupambana na mimba shuleni, pia katika vikao vyetu vya maendeleo ya kata kama madiwani na mikutano ya hadhara ya vijiji na kata, tunaendelea kuhamasisha jamii kutoa elimu, na kuonyesha madhara ya kubeba mimba shuleni," anasema.

Hata hivyo, Evata anasema bado kuna changamoto ya kukosa ushirikiano kutoka kwa baadhi ya wazazi wa mabinti, kutotoa ushahidi dhidi ya mtuhumiwa hata baadhi ya kesi kuondolewa mahakamani.

"Wazazi wa watoto wanakutana kimya kimya wanakubaliana, na wakati mwingine wazazi wa binti wanapewa hela ili waue kesi," anadokeza kinachofanyikia kwa siri," anasema.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kanisa la KKKT, Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, migogoro ya ndoa inaendelea kuongoza katika jamii, ikilinganishwa na migogoro mingineyo inayoripotiwa katika kitengo hicho.



Mratibu wa Vijana katika Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Lweru, Mchungaji Hosseah Baraseka. **PICHA: LILIAN LUGAKANGIRA.**

**KUTOKA NGO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Mashirika yanayotoa Msaada wa Kisheria Christina Ruhinda, anasema wameanzisha klabu zinazozungumzia ukatili wa kijinsia, upatikanaji haki na huduma za kisheria, ili kukabili mimba za mabinti shuleni.

Anasema klabu hizo zimesaidia watoto kutoa na kupokea taarifa za changamoto zinazowakabili na wanageuzwa mabalozi wa kutoa elimu na kudhibiti masuala ya mapenzi, kwani ni kinyume cha sheria kwao.

Kuhusu watoto kupata mimba na kurejeshwa shuleni anasema ni fursa nzuri kwao, anasema wengi wanaokumbana na tatizo hilo, pindi wanarudi masomoni wanakuwa na kasi kubwa ya kusoma, maana wanakuwa tayari wamejifunza na kujutia magumu yaliyowakuta.

"Ule moto anaopitia binti aliyepata ujauzito akiwa shuleni ni funzo kubwa maana wazazi, ndugu na jamaa wanamkataa, wanafunzi wenzake wanamnyanyapaa anabaki mpweke, kwa hiyo hilo 'joto la jiwe' analolipitia sio mchezo linamfanya abadilike," anasema Christina.

Anawaasa wazazi kutowatenga watoto waliopata ujauzito wakiwa shuleni baada ya kujifungua, badala yake waendeleze ushirikiano na kuwasimamia ipasavyo.

**ALIYEFIKWA AFUNGUKA**

Olvia (jina la pli tunalo) mwenye umri miaka 19, mkazi wa wilayani Muleba, anayejitambulisha anatoka kwenye familia yenye mgogoro na hata kuchangia kupata ujauzito hadi kufukuzwa shule mwaka huu akiwa kidato cha nne.

Anasema hadi sasa ni zaidi ya nusu mwaka tangu kufukuzwa shule, lakini anashukuru wazazi hawajamfukuza, ingawa anakiri mateso ya kutegemea matumizi ya kipato duni cha mama yake.

Pia, anadokeza mimba yake ni zao la migogoro ya kifamilia, kati ya mama na baba yake, iliyowakosesha muda wa kumsikiliza na kutatua shida zilizomkabili, hata akakata tamaa na kutafuta faraja mbadala, iliyomuingiza shimoni.

"Hata nilipopata tatizo nilikosa wa kumshirikisha. Baba ni msumbufu na mtu wa kuondoka na kurudi nyumbani usiku sana. Hali hii humfanya mama kuwa na wakati mgumu kiasi kwamba sio rahisi kusikiliza matatizo ya mtu mwingine," anasema.

Anasema katika maisha yake alitamani kuwa askari hasa wa Usalama Barabarani, lakini sasa amekata tamaa ya kufikia ndoto hiyo.

"Baada ya kujifungua nikipata mtu wa kunisaidia niko tayari kuendelea na masomo, nimezungumza na mama yangu ameniahidi nikijifungua salama yuko tayari kubaki na mtoto nami niende kusoma.

Mhusika wa ujauzito? Olvia, mtoto wa tatu katika familia anasema tangu alipomweleza alitoweka na hafahamu aliko. Alikuwa akijihusisha na kilimo kijijini kwao.

AFYA

# Unatumia tumbaku? Zijue sumu zake zinavyojificha mwilini na kukumaliza

## • Sekunde kadhaa kwenye ubongo
## • Jirani na mvutaji, hatari yake ileile

**Na Sabato Kasika**



KATIKA taarifa kwenye maadhimisho ya Siku ya Kutokuvuta Tumbaku Duniani, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anasema takribani watu milioni sita hufariki dunia kila mwaka duniani kutokana na matumizi ya tumbaku au kukaa karibu na mvutaji.

Pia, anageukia nchini na kusema, wastani wa asilimia 14 ya Watanzania wanatumia tumbaku na kwamba idadi ya wanaoathirika kutokana na moshi wa tumbaku kutoka kwa wavutaji inaongezeka.

Waziri anafafanua kuwa asilimia 17.5 duniani huathiriwa na wanaovuta sigara majumbani na asilimia 24.9 ni katika sehemu za kazi. Hapo anaiasa jamii izingatie kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu 'dhamiria kuacha kutumia tumbaku na bidhaa zake.'

Ili kuendelea kudhibiti bidhaa tumbaku, wizara hiyo imeidhinisha Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), jukumu la udhibiti bidhaa hizo ili kuiokoa jamii.

Mkurugenzi wa TMDA, Adam Fimbo, anasema ni hatua zinazochukuliwa kwa sababu tumbaku inahusishwa na magonjwa yasiyoambukiza, watu wengi wakiathirika.

**INAVYODHIBITIWA**

Fimbo anasema kazi yao ni kusimamia upunguzaji watumia tumbaku, vilevile kuhakikisha idadi ya watumiaji wapya inashuka.

"Katika muktadha huo, watoto wenye umri chini ya miaka 18 ambao sheria inakataza wasuvute sigara, TMDA inaweka mazingira ya kuhakikisha kwamba hawatumbukii kwenye uvutaji wa sigara au kula ugoro," anasema Fimbo.

Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa mamlaka yake imeanza kutengeneza utaratibu wa namna watadhibiti soko, kwa maana ya kuangalia jinsi watakavyosajili bidhaa tumbaku.

"Sheria inataka kutengwa maeneo kwa ajili ya uvutaji sigara kama vile kwenye kumbi za starehe, baa, mikusanyiko ya watu hotelini na kadhalika.

"Pia, mamlaka ina kazi ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna sahihi ya kuvuta sigara, ikiwamo mazingira na athari za bidhaa hizo," anasema.

Fimbo anasema, mamlaka yake iko kwenye utaratibu wa kuweka mfumo bora wa utumiaji bidhaa za tumbaku, lengo ni kufanikisha wanapunguza madhara kadri inavyowzekana.

**KUMALIZA TATIZO?**

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Kudhibiti Tumbaku Tanzania (TTCF), Lutgard Kagaruki, anasema ni njia itakayowafanya Watanzania kubaki salama, waachane na ulimaji tumbaku.

Anasema yapo mazao yanayoweza kuwa mbadala wa tumbaku kama karanga, ufuta, alizeti na chai, ambayo yakipewa kipaumbele yanawaongeza kipato waliokuwa wakilima tumbaku.

Kagaruki anasema, utafiti umeonyesha ni mazao yanayoweza kuwa mbadala na yana maslahi zaidi ya tumbaku, pasipo kuathiri afya za umma.

"Kwenye suala la uvutaji sigara, sheria inataka yatengwe maeneo kwa ajili ya wavutaji, ila sisi tunaamini kwamba hiyo si njia sahihi, kwani haipendezi kutengea watu maeneo waende kujiua," anasema Kagaruki.

Anashauri matangazo yote ya sigara katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii yaondolewe, kwa kuwa yanachangia kushawishi vijana kujiingiza kwenye uvutaji tumbaku katika umri mdogo.

"Inasikitisha kuona au kusikia matangazo yanayoshawishi watu kutumia bidhaa za tumbaku bila kujali kwamba ni tatizo na bahati mbaya unaweza kukuta baadhi ya vijana wakivuta wangali wadogo," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema baada ya serikali kuagiza kampuni zinazotengeneza sigara kuweka matangazo ya onyo kwenye pakti, yakiwekwa madogo, ambayo ni vugumu mtu kuyagundua kirahisi

**DAKTARI NA YAKE**

Francis Furia, Daktari Bingwa wa Magonjwa, pia Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Tiba Muhimbili, Dar es Salaam, anasema mvutaji sigara anadhurika maradufu kuliko asiyevuta, ingawa anayepokea moshi hayuko salama.

Ana ufafanuzi:"Kemikali za moshi wa sigara huingia katika mapafu na kuenea mwili mzima na kuleta madhara makubwa kwa njia mbalimbali, mvutaji anaweza kupata magonjwa ya moyo, kiharusi, saratani ya mapafu, matatizo katika mfumo wa kupumua yanayojulikana kama COPD."

Dk. Furia, ambaye pia yumo katika Chama cha Wataalamu wa Magonjwa ya Watoto (PAT), anataja magonjwa mengine ni ya mishipa ya damu, watoto kuzaliwa njiti au uzito kidogo na shinikizo la damu.

Anatoa mfano wa kimelea nikotini huufikia ubongo ndani ya muda sekunde saba hadi 10, baada ya moshi wa sigara kuvutwa na kemikali hiyo hutapakaa sehemu nyingi za mwili, ikiwamo maziwa ya mama.

"Nikotini ni kemikali sumu ambayo kwa muda mrefu inatumiwa kama dawa ya kuua wadudu na sumu ya panya. Inachukua nafasi ya pili kama sumu kali kabisa kutokana na athari yake mbaya kwa mwili wa binadamu," anaeleza.

Dk. Furia anataja kemikali nyinginezo kwa jina la 'tar', kwamba inasababisha saratani mwilini na hupatikana katika tumbaku inayoharibu nyenzo ya kimwili 'jeni; ambayo ni muhimu kuzuia ukuaji holela wa seli zisiwe za saratani.

Kimsingi, jeni ni mahali ambako DNA inapatikana mwilini. Aidha, DNA hiyo maana yake ni mkusanyiko wa taarifa za kemikali zinazobeba maelekezo ya kutengeneza protini kwenye chembe hai.

Mtaalamu huyo anaendelea akitaja hewa ana ya 'carbon monoxide' anaifafanua: "Ni gesi yenye madhara inayopatikana katika moshi wa sigara ambayo hujishikiza ndani ya seli nyekundu za damu na kuzizuia zisibebe vyema hwa inayohitajika ya oksijeni.





## Watafiti wapewa maeneo 12 sekta kilimo kutafiti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATAFITI wametakiwa kufanyia utafiti maeneo 12 katika sekta ya kilimo nchini ikiwamo uboreshaji wa mazao kwa kugundua mbegu mpya ili kuleta tija kwa sekta hiyo.

Mkurugenzi mstaafu wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Dk. Everina Lukonge aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa mada ya kutambua maeneo muhimu ya kufanyia utafiti wa kilimo nchini kwenye Mkutano wa Kitaifa wa wadau wa utafiti kwenye kilimo (NARA) ambao unalenga kutengeneza ajenda ya utafiti kwenye maendeleo ya kilimo.

Alisema kwasasa kuna maeneo 12 ya kufanyia utafiti na la kwanza ni uboreshaji wa mazao ili kufanya kilimo kuwa na tija na maeneo madogo ya kufanyia utafiti ikiwamo ugunduzi wa mbegu mpya.

"Katika uboreshaji wa mazao kwa kuangalia kilimo chetu kiwe na tija, tumesema kuboresha mazao kunahitaji utafiti na hii ripoti ya maeneo haya si kwa ajili ya watu wa TARI pekee bali ni watafiti wote nchini wawe binafsi, vyuo yeyote anayefanya utafiti kwenye kilimo inamhusu," alisema.

Alibainisha katika eneo hilo linahitaji ugunduzi wa mbegu mpya kwa kuangalia mambo mbalimbali ikiwamo masoko.

Aidha, alisema eneo jingine katika uboreshaji huo ni lazima ukusanyaji vinasaba ili kuboresha, upatikanaji wa mbegu bora kwa ajili ya vizazi vijavyo na vya sasa.

"Kuna eneo la kilimo uchumi, mabadiliko ya tabia nchi, kilimo hifadhi, kilimo mseto, masoko, kusambaza teknolojia, kufanyia kazi sayansi mpya ambazo tumegundua sisi na zilizogunduliwa na wengine," alisema.

**Alibainisha katika eneo hilo linahitaji ugunduzi wa mbegu mpya kwa kuangalia mambo mbalimbali ikiwamo masoko.**

# Anwani makazi zafikia asilimia 3 kata zote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, amesema hadi kufikia mwezi huu asilimia tatu ya kata zote zilizopo nchini zilikuwa zimefikiwa na huduma ya anwani ya makazi.

Alizitaka halmashauri kushiriki ipasavyo kwenye jukumu hilo ili kata zote zifikiwe na huduma hiyo.

Dk. Kijaji aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua semina ya kujenga uelewa na kuhamasisha utekelezaji wa mfumo wa anwani za makazi kwa Jumuiya ya Serikali za Mitaa.

Alisema asilimia hiyo tatu ni ya kata 135 kati ya 4,067 zilizopo nchini na kwa Zanzibar zipo 110.

"Ni wajibu wetu kusema sisi ni wana mabadiliko tunakwenda kushiriki kwenye jukumu hili, nimshukuru Rais wetu Samia Suluhu Hassan amesema kama tatizo ni pesa, nitatoa ili kufikia lengo hili," alisema.

Alisema Wizara ya Habari imepewa Sh. bilioni 45 kwa ajili ya uratibu wa kuweka anwani hizo huku Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ikipewa zaidi ya Sh. bilioni 100 na kuwataka viongozi hao kusafiri kwa pamoja kukamilisha kazi hiyo.

"Sisi kama waratibu tunasema tutasafiri na yule atakayekuwa na kasi kwenye utekelezaji, twende kwa pamoja, tusafiri kwa pamoja, Wizara ya Ardhi wapo tayari kwenye kupima," alisema.

Alifafanua kuwa mfumo huo unarahisisha wananchi kushiriki moja kwa moja kwenye shughuli za maendeleo ya kijamii.

"Dunia yetu kwasasa inaelekea kwenye uchumi wa kidigitali, kuna kufanya biashara kwa njia ya mtandao, unafanya mawasiliano kwa njia ya mtandao na unaletewa bidhaa yako hadi nyumbani," alisema.

Alisema hatua hiyo itasaidia kukuza uchumi kwa kuwa Watanzania hawatapoteza muda wao kufuatilia bidhaa au huduma.

"Twendeni tukawashirikishe madiwani kila mmoja akashirikishe jamii yake, watendaji wa kata, vijiji, mitaa ili kufikia haya, Tanzania imeamua kuingia kwenye dunia ya kidigitali," alisema.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema wamejipanga ifikapo mwaka 2025 kuhakikisha kila nyumba inakuwa namba yake.

"Kwa kila Mamlaka za Serikali za Mitaa kila Mkurugenzi ana hii bajeti, lakini utekelezaji wake ni wa kusuasua, Halmashauri ya Jiji la Mwanza imefanya kazi kubwa," alisema.

Awali, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, alisema zimeandaliwa sheria ndogo zitakazotumiwa na halmashauri kusimamia utekelezaji wa mfumo huo wa anwani za makazi.

Alisema postikodi zote zimeandaliwa na kuingizwa kwenye kanzidata, halmashauri 21 zimeshajengewa uwezo juu ya maudhui ya mfumo huo.

"Imeandaliwa mfumo wa kitaifa wa anwani za makazi...imeandaliwa program tumizi kwa ajili ya kuhakikisha utoaji huduma za kiuchumi na kijamii pamoja na kusimamia utoaji wa huduma, rasimu ya utekelezaji wa mfumo huu umeandaliwa," alisema.

Alibainisha kuwa shughuli za uingizaji wa anwani ya makazi zimeingizwa kwenye mwongozo wa bajeti na kuhimiza Halmashauri kutenga fedha kwa ajili hiyo.




Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Lilian Badi, akiwasalimia wajumbe wa mkutano mkuu wa mwaka wa mashirika hayo, uliofunguliwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watoto waathirika wakuu kung'atwa na mbwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAATHIRIKA wakuu wa ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni watoto chini ya miaka 15 kutokana na kucheza au kuchokoza mbwa wasiowafahamu njiani.

Takwimu zinaonesha kuwa ugonjwa huo unakadiriwa kusababisha takribani vifo 59,000 duniani na asilimia 36 ya vifo hivyo hutokea katika Bara la Afrika huku kati ya asilimia 30 hadi 50 ya waathirika wa ugonjwa huo ni watoto chini ya miaka 15.

Kwa hapa Tanzania, kati ya mwezi Januari hadi Agosti mwaka huu, watu 39,787 wameng'atwa na mbwa huku mikoa ya Morogoro na Dodoma ikiongoza kwa matukio hayo.

Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia magonjwa yasiyoambukiza wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. James Kiologwe, aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akitoa tamko la siku ya kichaa cha mbwa kwa niaba ya Mganga Mkuu wa serikali.

Alisema takwimu hizo kwa Tanzania zinaonesha ongezeko la zaidi ya watu 5,000 ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Alieleza kuwa matukio yaliyoripotiwa ya watu kuumwa na mbwa au wanyama wa jamii hiyo kwa Mkoa wa Morogoro ni 4,329 na Dodoma ni 4,233.

"Takwimu hizi hazijumuishi matukio yaliyotokea katika vituo vya kutolea huduma bila kutolewa taarifa au yaliyotokea nyumbani na waathirika ambao hawakufika katika vituo vya kutolea huduma za afya, hivyo tatizo hili ni kubwa kuliko tunavyofikiri," alisema.

Pia, alisema utafiti uliofanyika mwaka 2002 ulibainisha kuwapo na uwezekano wa takribani vifo 1,499 kwa mwaka nchini kutokana na ugonjwa huo.

"Kama tulivyoona hapo juu kuwa waathirika wakuu wa ugonjwa huu ni watoto chini ya miaka 15 na hii ni sababu wao ndio wanaokuwa karibu na mbwa muda mwingi na pia hupenda kucheza au kuchokoza mbwa wasiwafahamu njiani," alisema.

Alisema serikali inachukua jitihada mbalimbali za kudhibiti ugonjwa huo kwa kutoa elimu kwa umma, kuboresha dhana ya afya moja nchini, kurahisisha upatikanaji wa huduma za chanjo ya kichaa cha mbwa kwa wananchi na kurahisisha upatikanaji wa huduma za chanjo kwa wanyama hasa mbwa.

Hata hivyo, alisema serikali inatambua gharama kubwa za upatikanaji wa chanjo na kupitia Wizara ya Afya, TAMISEMI na sekta nyingine zimechangia gharama za upatikanaji wa chanjo ili ziwafikie wananchi kwa gharama wanayoimudu.



# H'mashauri Rungwe yatoa mil. 201/- ujenzi wa kituo

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya imetoa Sh. milioni 201 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kinyala ili kusogeza karibu huduma za matibabu hususani za mama na mtoto.

Fedha hizo zinatokana na mapato ya ndani ya halmashauri hiyo na jumla ya vijiji sita vya Kata ya Kinyala vitanufaika na uwapo wa kituo hicho.

Akizungumza jana na wakazi wa eneo hilo, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, alisema jumla ya wananchi 16,964 na wengine kutoka Wilaya ya Mbeya watanufaika na huduma za matibabu katika kituo hicho.

"Naagiza kila mkazi wa kata hii ashiriki kikamilifu kuchangia nguvu kazi ili kupunguza gharama za ujenzi na fedha itakayobaki itumike katika ukamilishaji wa miundombinu mingine," alisema Dk. Anney.

Aliwaonya wananchi kutojihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi wa kituo hicho ili kutokwamisha ukamilishaji wa mradi huo kwa wakati.

Vilevile, aliwasisitiza wananchi kuendelea kupata chanjo ya corona ili kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo.

Kadhalika aliwataka kushiriki sensa ambayo inatarajiwa kufanyika hivi karibuni kwa kutoa taarifa sahihi na kuipa nafasi serikali kupanga shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na utoaji huduma stahiki kwa wananchi wake.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Rungwe, Antony Mwantona, ameahidi kuchangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Msingi Kisoko na Kasumba pamoja na mabati 100 kwa Sekondari ya Kinyala ikiwa ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoka hivi karibuni.

Alisisitiza kuwa kituo hicho kitakuwa na majengo ya wagonjwa wa nje (OPD), jengo la mama na mtoto pamoja na vyoo, vichomea taka na miundombinu mingine itaendelea kadiri ya upatikanaji wa fedha.




Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Mbeya (Uchumi), Said Madito, akizungumza na wafanyabiashara kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, katika kikao cha kujadili namna ya kuzitumia fursa zinazopatikana ndani na nje ya nchi kupitia Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Wananchi Ilemi kuondolewa adha ukosefu kituo cha afya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JUMLA ya Sh. milioni 524.6 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Ilemi ili kuwaondolea adha wakazi wa eneo hilo kutumia muda na gharama kufuata huduma hiyo maeneo mengine.

Kwa historia Kata ya Ilemi haijawahi kuwa na kituo cha afya na kwamba kukamilika kwa ujenzi kutawasaidia wananchi kupata huduma za matibabu kwa wakati.

Akizungumza na Nipashe Meya wa Jiji la Mbeya, Door Issa Mohamed, alisema katika kukafanikisha ujenzi huo, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, imetenga Sh. milioni 200 kutoka kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mohamed alisema kituo hicho kinatarajiwa kujengwa kwa gharama ya Sh. milioni 524.6 kwa awamu ya kwanza na kwamba fedha zitaendelea kutolewa kadiri zitakavyokuwa zinapatikana kutoka kwenye vyanzo mbalimbali.

"Tutakijenga kituo hiki kwa kutumia utaratibu wa Force Account hivyo nawaomba wananchi mjitokeze kujitolea kufanya kazi hapa maana utaratibu huu unataka sana ushiriki wa wananchi kwenye utekelezaji," alisema Mohamed.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa jiji hilo, Amede Ng'wanidako, aliwataka wananchi kuendelea kulipa kodi na tozo mbalimbali zinazotozwa na serikali ili fedha za kutekeleza mradi huo pamoja na miradi mingine zipatikane.

Alisema ili kufanikisha miradi kila Mtanzania anatakiwa kuchangia kwa kulipa ushuru na kodi na kuepuka kutegemea misaada kutoka nje ambayo kwa kiwango kikubwa huwa na masharti magumu.

# Viongozi wa kimila, dini wahamasisha chanjo corona

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

VIONGOZI wa kimila na dini kutoka Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamewasisitiza wananchi kujitokeza kupata chanjo ya ugonjwa wa corona ili kujikinga na kuwakinga wengine.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Chifu wa Kabila la Wasangu, Salehe Merere baada ya kupata chanjo ya corona na kuwahamasisha wananchi kujitokeza kuchanja ili kuunga mkono jitihada za serikali kukabiliana na ugonjwa huo hatari.

Alisema moja ya kikwazo kinachosababisha mwitikio mdogo kwa wananchi ni elimu na kampeni inayoendelea kwa sasa kuhamasisha wananchi itaongeza idadi ya wengi kupata chanjo. Aliwasisitiza kuacha kusikiliza maneno ya upotoshaji yanayotolewa na baadhi ya watu wakidai zina madhara kiafya ilhali zimethibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) pamoja na wataalam wa afya nchini.

"Awali nilikuwa miongoni mwa viongozi waliokuwa wakipingana na jambo la chanjo kutokana na kukosa uelewa wa kutosha juu ya jambo hilo maneno ya mganga wetu mkuu wa wilaya yametosha," alisema Merere.

Kwa upande wake Shekhe Mkuu wa wilaya hiyo, Ayubu Biski, aliwataka Waislamu kuchukua tahadhari kwa kuwa hawakuzuiwa katika masuala ya mlipuko kuweka kinga wala kuweka karantini na hiyo ilikuwapo tangu wakati wa mtume.

Aliviomba vyombo vya dola wilayani hapa iwapo atatokea imamu wa msikiti wowote kati ya 86 iliyopo kusimama na kuhubiri kukataa watu kuchanja, viwasiliane na viongozi wa dini hiyo ngazi ya wilaya ili wawape elimu kwakuwa wao wenyewe wameelewa na kuridhia kuchanjwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune alisema yapo mambo matatu yaliyoonekana kukwamisha suala la chanjo moja ikiwa ni pamoja na viongozi kutotaka kuonyesha njia kwa wanaowaongoza.

Baadhi ya watumishi wa umma wakiwamo wa sekta ya afya kutochanja, aliagiza Mganga Mkuu na viongozi wenzake kukaa pamoja na kutafakari suala hilo.

Pia aliagiza baada ya kikao hicho kuundwa kwa kamati zitakazojumuisha wataalamu, viongozi wa kidini na serikali zitakazopita kila kata kwa muda wa siku tatu kwaajili ya kutoa elimu juu ya chanjo kama iliyotolewa kwenye kikao hicho na kisha kuleta mrejesho kwake.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa chanjo, Mganga Mkuu wa wilaya, Godfray Mwakalila, alisema kwenye mgawo wa kwanza wilaya ilipata dozi 8,500 hadi kufikia juzi dozi 1,358 zilitolewa kwa wananchi.

Alisema dozi 152 ziliharibika baada ya kufunguliwa kutokana na wateja kutokuwapo kwa wakati hadi muda wake unamalizika na dozi 6,990 ndizo zimesalia.



# Majengo 20 yaliyopo Mji Mkongwe yapangishwa kuyanusuru

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya majengo 20 yaliopo katika Mji Mkongwe wa Zanzibar yakiwamo yanayomilikiwa na serikali na watu binafsi yamekodishwa kwa watu na wawekezaji ikiwa ni hatua ya kuyaendeleza kwa kuyafanyia ukarabati ili kuepuka tishio la kuanguka.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohamed Mussa, alisema hayo wakati akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani na kusema serikali imejipanga kuhakikisha mji Mkongwe unabaki kuwa utambulisho wa mji wa Zanzibar kutokana na kuwapo kwa historia nyingi ya mambo ya kale.

Alisema majengo mengi yaliyopo katika Mji Mkongwe yamebeba historia kubwa ya mambo ya kale ambayo yanatakiwa kuenziwa na kulindwa kwa faida ya vizazi vijavyo.

Aliwataka wananchi ikiwamo wakazi wa mji huo kuendelea kuchukua juhudi za kuulinda ikiwamo hifadhi yake ya urithi wa mambo ya kale.

"Wakati Zanzibar tukiadhimisha Siku ya Utalii Duniani tumejipanga kuhakikisha Mji Mkongwe unabakia na haiba yake na hadhi ya miji ya kihistoria ya urithi wa mambo ya kale duniani kwa kuyafanyia ukarabati majengo hayo," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendeshaji wa Mji Mkongwe, Madina Ali Khamis, alisema juhudi za kulifanyia ukarabati jengo la Beit Al-Jaib ambalo lilianguka mwaka jana zinaendelea kwa ushirikiano na taasisi mbalimbali za kimataifa zinazojishughulisha na uhifadhi wa miji ya kihistoria duniani.

Alisema bado nia ya Serikali ya Oman kulifanyia ukarabati jengo hilo ipo na kazi inayofanywa kwa sasa ni kulihifadhi ili lisipate athari nyingine na kusababisha kuporomoka zaidi.

**Aliwataka wananchi ikiwamo wakazi wa mji huo kuendelea kuchukua juhudi za kuulinda ikiwamo hifadhi yake ya urithi wa mambo ya kale.**

# Mwinyi asema serikali yake haina ukabila wala dini

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa anaiendesha Serikali ya Zanzibar bila ya ubaguzi wa kidini, rangi wa kabila na kwa kufuata misingi ya Katiba na sheria.

Alisema hata teuzi zake za viongozi mbalimbali katika serikali haufanyiki kwa misingi ya dini, jinsia wala rangi isipokuwa vigezo na sifa ndiyo kitu cha msingi kinachozingatiwa.

Akizungumza jana na viongozi wa dini ya Kikristo huko Welezo Mjini Unguja, Dk. Mwinyi, alisema yupo tayari kupokea majina ya vijana wenye sifa ambao wana uwezo wa kuongoza nafasi mbalimbali serikali kutoka katika makundi ya Wakristo ili anapofanya teuzi nao wawemo.

"Nileteeni majina ya vijana wenye uwezo na sifa za kielimu ili tuwachaguwe kushika nafasi mbalimbali za uongozi...vigezo vya uteuzi wa nafasi mbalimbali za uongozi sifa yake kubwa ni uwezo na sio misingi ya dini au kabila wa mtu anatoka wapi iwe kusini au kaskazini," alisema.

Aidha, alisema ameunda serikali ya umoja wa kitaifa kwa ajili ya kuwaunganisha wananchi wote hatua ambayo imesaidia kuondoa siasa za chuki na uhasama.

Alisema hatua iliyofikiwa sasa hakuna sababu ya wananchi kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa ikiwamo uchumi wa bluu na uwekezaji.

"Serikali ya Umoja wa Kitaifa imewaunganisha wananchi wote na kwa kiasi kikubwa kuondoa malumbano ya kisiasa na uhasama...nashukuru sana hatuna sababu kwa nini tushindwe kuyafikia malengo tuliyojiwekea kwa sababu amani tunayo na utulivu wa kidini," alisema.

Akijibu hoja na malalamiko ya viongozi wa dini kuhusu masuala ya nyumba za ibada kati ya Waislamu na Wakristo na kusababisha migongano inayotishia uvunjifu wa amani, aliwataka watendaji wa mipango miji kuweka ramani vizuri ya mipango miji ili kutenganisha makazi hayo na kuepuka malalamiko.

Alisema lipo tatizo la ukosefu wa maeneo ya kuzikana katika mji wa Zanzibar kwa sababu watendaji wa mipango miji wameshindwa kutenga maeneo hayo.

"Nimewaagiza watendaji wa mipango miji kutenga maeneo ya kuzikana binadamu pamoja na maeneo ya kufanya ibada kwa lengo la kuondoa malalamiko kati ya waumini wenye dini tofauti," alisema.

Viongozi wa dini walitoa malalamiko yao mbele ya Rais wa Zanzibar kuhusu uteuzi wa nafasi za uongozi ikiwamo za kisiasa kutotoa nafasi kwa makundi mengine ya dini hasa ya kikristo.

Pia, walilalamikia nafasi za ajira serikalini na kutopatiwa vibali vya ujenzi wa nyumba za ibada katika maeneo mbalimbali ya mji huo jambo ambalo ni changamoto kubwa.

"Tunamasikitiko makubwa kuhusu suala la ajira hatupati nafasi, lakini tunapotaka kujenga nyumba za ibada kuna ukiritimba mkubwa katika kupata kibali cha ujenzi," alisema Askofu wa Kanisa la Kiluthen Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Zanzibar, Shukuru Maloda.

Naye Askofu wa Kanisa la Katoliki Zanzibar, Agostino Shao, amempongeza Rais wa Zanzibar kwa juhudi anazozichukua za kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo ubakaji kwa kukemea kwa kauli zake na kuonyesha vitendo.

Alisema kanisa limefanya kazi ya utafiti kuhusu vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia katika baadhi ya miradi yake na kubaini lipo tatizo kubwa ambalo ni tishio kwa mustakabali wa watoto na wananchi kwa ujumla.

"Sisi kanisa tunaunga mkono juhudi zako za kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo kuunda mahakama maalumu za kushughulikia kesi za ubakaji kwa haraka... juhudi zako ni sahihi," alisema Mwenyekiti wa Baraza la Maskofu Zanzibar Agostino Shao.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Viongozi wa Madhehebu ya Dini ya Kikristo, mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali kuziboresha shule sekondari kwa kuzikarabati

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis, amesema wanatarajia kuzifanyia ukarabati shule za sekondari ili kutoa nafasi kwa wanafunzi kuendelea na elimu katika mazingira bora.

Aliyasema hayo juzi wakati wa utiaji saini wa ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Mtule Paje Wilaya ya Kusini Unguja na Kampuni ya Rans, ofisini kwake Mazizini Mjini Zanzibar.

Katibu mkuu huyo alisema serikali imejipanga vizuri kuimarisha mazingira ya elimu kwa wanafunzi wa shule za sekondari Unguja na Pemba na kuzipatia vifaa vya maabara na madawati.

Alizitaja miongoni mwa shule zingine zitakazofanyiwa ukarabati ni Sekondari ya Chwaka na Tumbe Mkoa wa Kaskazini Pemba ili zirudi katika ubora wake na kutoa huduma bora ya elimu.

"Wizara ya Elimu itaendelea na zoezi la kufanya ukarabati wa shule ambazo zipo katika hali mbaya ya uchakavu kiasi ya wanafunzi wake kukosa utulivu.

Alisema tayari ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Wanawake ya Ben Bella iliyopo Mji Mkongwe umekamilika na kinachosubiriwa ni kukabidhiwa wizara.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Rans, Yunus Ali Gare, alisema ukarabati wa shule hiyo unatarajiwa kuchukua takriban miezi sita hadi kukamilika na kuhusisha maeneo ya mapaa ambayo yanavujisha maji.

Alisema watafanya ukarabati wa shule hiyo kwa mujibu wa mkataba wao na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kumalizika kwa wakati ili kutoa huduma za kupokea wanafunzi.

"Kampuni yetu tunaahidi kufanya kazi kwa ufanisi na kukidhi malengo na matarajio ya ukarabati wa shule hii na kuhakikisha athari zote zilizojitokeza zinafanyiwa kazi," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA IPO MWANANYAMALA KWA KOPA. INA VYUMBA VITATU VYA KULALA, SEBULE, JIKO, CHOO NDANI NA NJE. INA UMEME, MAJI NA FENCE. KWA MAWASILIANO PIGA: 0754409991.

MFAMASIA ANAHITAJIKA

ANAHITAJIKA MFAMASIA MWENYE LESENI YA BODI MADUKANI PHAMACY SINZA DAR ES SALAAM. SIMU NAMBA 0745 181910.

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**SCHOLASTICA MARWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0540/021** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAPOSENI SEKONDARI mwaka 1990.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **MUL/RB/922/2019.**

116483002

## Tangazo kupotea Ofa ya Kiwanja

**Theresia Mathew** mkazi wa Ngokolo Shinyanga. Anatangaza kupotelewa na Ofa ya Kiwanja namba **87 Kitalu "FF"** kilichopo Ngokolo Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Theresia Mathew kwa simu namba **0754-431308.** **Rb namba/SHY/RB/2021/** Control namba **9910830402202.**

116483102

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 106 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DAVID MWALIMU NYAKAPALA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MSAFIRI DAVID MWALIMU**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **26 Day of October, 2021.**
Dated at Dodoma this **1st day of September 2021** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAPOSENI SEKONDARI mwaka 1990.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **MUL/RB/922/2019.**

MAGISTRATE RESIDENT MAGISTRATE


116483202

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha DODOMA MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na…/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU KAUNDIME RAMADHANI BARUANI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA FATUMA SALEHE LUKINDO**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama ya mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo **tarehe 04/11/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo **tarehe 16/09/2021**

116483302

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA VYETI



Ndugu Michael Maclean Mbonile Anatangaza kupotelewa na Vyeti vya Elimu ya Sekondari, Cheti cha kidato cha Nne Nambari S2421-0038 kilichotolewa na Shule ya STAR SEKONDARI na Cheti cha kidato cha Sita Nambari S0692-0659 kilichotolewa na Shule ya ROSMINI SEKONDARI
Vyeti hivi vilipotoea tarehe 29/04/2021 akiwa safarini kutoka Arusha kwenda Dar Es Salaam kwa basi la Dar Express ambalo lilipata ajali eneo la Maili sita, Korogwe Tanga
Kwa atakaeviona tafadhali viwasilishe katika kituo chochote cha polisi
(RB NO. ARU/ARU/RB/456780 & ARU/ARU/RB/456778)

116483502

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi NO.303/2021**

Ombi la **STELLAH MICHAEL TEMU** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **FADHILI SHABANI NDUJI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 07/10/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 23 /09/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENEDICT ELIABU MFURU** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 331 DSK – BMW. CHASSIS NAMBA WBAUF12020PZ34409. ENGINE NAMBA N45B16AEAA908988. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: ARU/ARU/RB/471577/2021.

116484402

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Usimamizi wa Mirathi No. 85/2021.**

**Ombi la JACKSON SAMSON ARON Kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu SAMSON ARON MKETA.**

Kwa **YEYOTE YULE ANAYEHUSIKA POPOTE PALE**
Watu wote wanadaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo TAREHE 01/10/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 31/08/2021.

Tarehe 31/08/2021
Sahihi ya Hakimu

116484502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha KINGOLWIRA**
**Mkoa MOROGORO**
**Shauri la Madai Na. 100/2021**

**Jina la Mdai** GRACE JOHN
**Jina la Mdaiwa** GELARD TEMBA

**KATIKA SHAURI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa GELARD TEMBA**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba ( Eleza hapa habari za madai) **MADAI YA PESA TSH.510,000/= PAMOJA NA GHARAMA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 04 mwezi 10 Mwaka 2021 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 09 mwaka 2021

HAKIMU MFAWIDHI MAHAKAMA YA MWANZO KINGOLWIRA MOROGORO.

116484602

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha DODOMA MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na.43/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MWANJAA BARORO wa AREA A**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SALIMU AZUBERI**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama ya mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 28/09/2021.

116484102

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wachuuzi bilioni nne duniani hawamo mifuko hifadhi ya jamii

**New York,** MAREKANI

ZAIDI ya watu bilioni nne duniani wakiwamo wachuuzi wa mitaani, hawana ulinzi wa kutosha wa hifadhi ya jamii Shirika la Umoja wa Mataifa la Kazi Duniani (ILO), limesema

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) António Guterres katika tamko lake la kisera lililotolewa jana, kuhusu ajira na ulinzi wa hifadhi ya jamii na kutokomeza umasikini, alisema dunia imeegemea kupambana na corona kwa miaka miwili na kusahau suala hilo.

Katibu Mkuu alisema uwekezaji katika ajira, ulinzi wa kijamii haswa katika nchi za kipato cha chini na cha kati, kunaweza kuzuia kuongezeka zaidi kwa pengo la usawa.

“Mshikamano wa kimataifa hadi sasa umekuwa duni kabisa. Mkataba mpya wa kijamii unapaswa kuwa kiini cha kujikwamua na janga hili.

“Umasikini uliokithiri umeongezeka miongoni mwa watu milioni 119 hadi milioni 224 kati ya Machi na Desemba mwaka jana, likiwa ni ongezeko la kwanza kwa zaidi ya miaka 21.”

Alisema kuwa zaidi ya robo tatu ya watu ni masikini wapya na wako katika nchi za kipato cha kati na kwamba utajiri wa mabilionea umeongezeka kwa zaidi ya dola trilioni 3.9.

ILO ilibaini kwamba kwa sababu ya janga la Covid-19, kuna upungufu wa wastani wa ajira milioni 75 mwaka huu, kuliko ilivyokuwa kabla ya janga hilo, ikiwa ni ajira milioni 23 chache zaidi ya zilizokadiriwa kwa mwaka 2022.

Pia ripoti inakadiria kuwa asilimia 8.8 ya jumla ya saa za kazi zilipotea mwaka jana, zikiwa ni sawa na saa zilizotumika na wafanyakazi milioni 255 kufanya kazi wakati wote kwa muda wa mwaka mmoja.

Ripoti ilisema, upotevu huo ni sawana upotezaji wa dola trilioni 3.3 za mapato ya wafanyakazi kabla ya msaada wa serikali.

Guterres alitaka ulinzi wa hifadhi ya jamii kwa wote ifikapo mwaka 2030, pamoja na huduma za afya kwa wote, ulinzi wa mapato, elimu na mafunzo ya ufundi, haswa kwa wanawake na wasichana.

“Lazima tuhamasishe uwekezaji mkubwa wa umma na wa kibinafsi takriban dola trilioni 1.2 kufikia ulinzi wa hifadhi ya jamii kwa nchi za kipato cha chini na cha kati,” alisema.

Pia alisema uwekezaji uwe na kiwango cha juu kusaidia kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na kushughulikia hatari za mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaweza kuhatarisha ajira bilioni 1.2, sawa na asilimia 40 ya nguvu kazi ya dunia.

Pia, Guterres alitangaza kuundwa kwa kichapuzi (Accelerator) kipya cha kimataifa cha ajira na ulinzi wa hifadhiyajamiikwaajiliyahakikatika wakati huu wa mpito wa kujikwamua na Covis-19, kwa kushirikiana na ILO.

Alisema ziundwe angalau ajira milioni 400 ifikapo mwaka 2030, haswa katika uchumi wa unaojali na kutunza mazingira, kupanua wa hifadhi ya jamii ifikapo 2025 hadi asilimia 50.

**UN**

# Wanajeshi wauawa operesheni dhidi ya ugaidi nchini Msumbiji

**Cabo Delgado,** MSUMBIJI

WANAJESHI wanne wa Rwanda wameuawa katika operesheni ya kijeshi dhidi ya wanamgambo wa kiislamu Msumbiji katika jimbo la Cabo Delgado, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Rwanda.

Hii ni mara ya kwanza kwa Rwanda kutangaza majeruhi katika kikosi chake cha wanajeshi 1,000 tangu waanze operesheni nchini Msumbiji.

Mbali na wanajeshi waliouawa, 14 wamejeruhiwa vibaya, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Rwanda.

Haijawekwa wazi ni katika eneo gani hasa la jimbo la Cabo Delgado, ambako wanajeshi wa Rwanda waliuawa.

Jumamosi iliyopita, marais wa Msumbiji na Rwanda, walikuwa wanawapongeza wanajeshi ambao wamejitoa kupambana na magaidi.

**BBC**


SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

## UNAUDITED RESULTS FOR THE SIX MONTHS ENDED 30 JUNE 2021

**Introduction**

**Dear Shareholders,**

We hereby present the unaudited trading results of Tanga Cement Public Limited Company (“Tanga Cement” or the “company”) and its subsidiaries (together, the “group”) for the six months ended 30 June 2021.

The half-year ending June 2021 was slightly more challenging than the comparative period in the prior year as described under the Financial and Operational Overview section below. We however affirm our commitment to all stakeholders through our high quality cement and clinker and our contribution towards the sustainable growth and development of Tanzania, a demonstration of our brand – “Strength Within”.

During the period the Company has been awarded the prestigious NOSA Certificate of Excellence for exceptional performance in managing Hazards and Risks at Workplace for the NOSA Northern Region. The focus remains to protect our employees and contractors by ensuring they continue to take pride in the work we do and how we do it.

**Macro-economic Overview**

The Group’s business growth continued to be anchored in the increased cement demand of the Tanzanian construction industry. The average annual headline inflation rate increased modestly to 3.6% for the year to date June 2021 from 3.2% for the full year ended 31 December 2020.

The Group remains optimistic of the positive impact of infrastructure development plans under the Government’s Development Vision 2025 programme, and expects the projects to continue gaining momentum throughout 2021 to 2023. The Group is confident with the measures that the Government has taken to stabilise the economy from the potential impact of COVD-19 and has committed to work with Government to ensure the health and safety of all our stakeholders.

Government expenditure data which shows that its capital expenditure about doubled from TZS 768.9bn (June 2020) to 1.532bn (June 2021) most of which went into infrastructure projects which strengthened the demand for cement.

The Group has capacity to meet a significant share of the cement demand in the country and remains committed to production of superior cement products.

**Financial and Operational Overview**

Group’s sales revenue increased by 14%, to TZS 107.2bn from TZS 94.3bn achieved in the comparative period to 30 June 2020.

Group’s cost of sales increased by 28% over the comparative period to 30 June 2020 mainly as a result of the purchase of 117,259.19 tons of clinker during the period to ensure sufficient cement production and supply to our customers whilst one of our major production units underwent major repairs and maintenance. This contributed to the decrease of the gross profit, EBITDA and operating profit achieved for the year to date 30 June 2021 compared to the same period in the prior year. The repairs to the production unit was concluded and commissioned ahead of schedule and we are confident that it will yield stable and sustainable production going forward at a relatively reduced production cost per ton.

The gross profit decreased by 27% to TZS 17.9bn from TZS 24.4bn in June 2020.

EBITDA decreased by 42% to TZS 9.6bn from TZS 16.7bn in June 2020 also being impacted by the 27% increase in operational maintenance related to the production unit, distribution and administration costs.

The Group recorded a loss before tax of TZS 11.4bn in June 2021 compared to the loss of TZS 5.1bn in June 2020, and a Net Loss after Tax of TZS 7.8bn in June 2021 compared to TZS 5.2bn in June 2020.

Cash generated from trading activities declined by 35% from TZS 16.5 billion recorded in June 2020 to TZS 10.6 billion in June 2021. Net cash flows from operations declined by 39% from TZS 16.0bn recorded in June 2020 to TZS 9.8bn in June 2021.

The Group continues to be committed to its sales, logistics and cost optimisation initiatives as it continually seeks to enhance value for its stakeholders. The Group remains positive about 2021 despite the very competitive landscape and the continued impact of COVID-19. Government initiatives to spur economic growth through infrastructure development and promotion of local industries will boost local cement output and consumption while reducing the influx of cheap imported cement.

**Dividend**

The company did not declare interim or final dividends to shareholders for 2021 and 2020 respectively in line with the financial performance for the year. The Board has decided to be prudent by committing available current cash resources to the operational and debt service commitments. The Board will evaluate the financial performance through 2021 financial year when considering dividend declarations.

**Conclusion**

The Board is grateful to management and staff for their passion and dedication to the company, and to its customers for their belief in the Simba Cement brand, as the company works to achieve its short- and long-term growth strategy.

With Tanzania remaining a significant player in the East African construction market, cement output is anticipated to increase and Tanga Cement is well positioned to take advantage of the growth opportunities in the regional market.

For and on behalf of the Board
**Lawrence Masha**
Chairman of the Board

| Consolidated and separate statements of profit or loss and other comprehensive income for the year ended 30 June 2021 | Group June 2021 TZS'000 | Group June 2020 TZS'000 | Company June 2021 TZS'000 | Company June 2020 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| **Revenue** | 107,152,122 | 94,326,912 | 107,152,122 | 94,326,912 |
| Cost of sales | (89,213,881) | (69,883,943) | (89,213,881) | (69,883,943) |
| **Gross profit** | 17,938,241 | 24,442,969 | 17,938,241 | 24,442,969 |
| **Other income** | 150,216 | 164,991 | 129,422 | 138,326 |
| Other expenses | (3,296,404) | - | (3,296,404) | - |
| Selling expenses | (1,600,995) | (1,435,278) | (1,600,995) | (1,435,278) |
| Administration expenses | (8,513,846) | (6,698,781) | (8,479,753) | (6,696,973) |
| Depreciation charge | (9,715,115) | (12,259,025) | (9,690,146) | (12,205,127) |
| Impairment and other charges | - | - | - | - |
| Expected credit losses (increase)/decrease | (141,500) | 180,463 | (210,375) | 231,544 |
| **Operating (loss)/profit** | **(5,179,403)** | **4,395,339** | **(5,210,010)** | **4,475,461** |
| Interest expense | (6,899,863) | (6,909,857) | (6,896,717) | (6,901,085) |
| Finance income | 945 | 3,159 | 945 | 3,159 |
| Foreign exchange and fair value losses | 637,713 | (2,575,217) | 631,283 | (2,575,217) |
| **Loss before tax** | **(11,440,608)** | **(5,086,576)** | **(11,474,499)** | **(4,997,683)** |
| Current income tax | (554,352) | (485,073) | (554,352) | (485,073) |
| Deferred tax credit | 4,198,245 | 397,363 | 4,198,245 | 397,363 |
| **Loss for the year** | **(7,796,715)** | **(5,174,286)** | **(7,830,606)** | **(5,085,393)** |
| Other comprehensive income | | | | |
| "Other comprehensive income to be reclassified to profit or loss in subsequent periods (net of tax):" | | | | |
| Exchange differences on translation of foreign operations | (7,993) | (18,630) | - | - |
| **Other comprehensive income net of tax** | (7,993) | (18,630) | - | - |
| **Total comprehensive income for the year, net of tax** | **(7,804,708)** | **(5,192,916)** | **(7,830,606)** | **(5,085,393)** |
| Loss for the year attributable to: | | | | |
| Owners of the parent | (7,796,715) | (5,174,286) | (7,830,606) | (5,085,393) |
| Non-controlling interests | - | - | - | - |
| | **(7,796,715)** | **(5,174,286)** | **(7,830,606)** | **(5,085,393)** |
| Total comprehensive income for the year attributable to: | | | | |
| Owners of the parent | **(7,804,708)** | **(5,192,916)** | **(7,830,606)** | **(5,085,393)** |
| **Non-controlling interests** | - | - | - | - |
| | (7,804,708) | (5,192,916) | (7,830,606) | (5,085,393) |
| **Weighted average number of shares in issue less treasury shares** | **62,967,893** | **62,967,893** | - | - |
| **Basic and diluted loss per share** | **-124** | **-82** | | |

| Consolidated and separate statements of financial position as at 30 June 2021 | Group June 2021 TZS'000 | Group June 2020 TZS'000 | Company June 2021 TZS'000 | Company June 2020 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| **Assets** | | | | |
| **Non-current assets** | | | | |
| Property, plant and equipment | 307,961,993 | 313,717,275 | 307,205,089 | 312,906,893 |
| Right-of-use assets | 5,018,425 | 10,187,786 | 4,763,337 | 9,908,648 |
| Investment property | 549,120 | 560,484 | - | - |
| Investment in subsidiary | - | - | 552,564 | 552,564 |
| Financial asset - Interest rate cap | 780,140 | 229,170 | 780,140 | 229,170 |
| Deferred tax asset | 2,291,395 | - | 2,291,395 | - |
| | **316,601,073** | **324,694,715** | **315,592,525** | **323,597,275** |
| **Current assets** | | | | |
| Due from employees' share trust | - | - | 351,575 | 351,575 |
| Inventories | 52,433,499 | 54,025,387 | 52,433,499 | 54,025,387 |
| Trade and other receivables | 11,603,747 | 9,799,677 | 12,009,320 | 9,948,423 |
| VAT recoverable | - | - | - | - |
| Current income tax recoverable | 6,856,578 | 6,443,707 | 6,320,584 | 5,969,790 |
| Cash and bank balances | 1,349,773 | 3,204,572 | 1,250,765 | 3,042,758 |
| | **72,243,597** | **73,473,343** | **72,365,743** | **73,337,933** |
| Non-current assets held for sale | 3,870 | 3,870 | - | - |
| **TOTAL ASSETS** | **388,848,540** | **398,171,928** | **387,958,268** | **396,935,208** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | | | |
| **Equity** | | | | |
| Issued capital | 1,273,421 | 1,273,421 | 1,273,421 | 1,273,421 |
| Translation reserve | (65,961) | (57,968) | - | - |
| Treasury shares | (351,575) | (351,575) | - | - |
| Retained earnings | 127,349,826 | 135,146,541 | 125,752,623 | 133,583,229 |
| **Equity attributable to owners of the parent** | **128,205,711** | **136,010,419** | **127,026,044** | **134,856,650** |
| Non-controlling interest | - | - | - | - |
| **TOTAL EQUITY** | **128,205,711** | **136,010,419** | **127,026,044** | **134,856,650** |
| **Non-current liabilities** | | | | |
| Lease liabilities | 7,589,163 | 5,160,608 | 7,599,938 | 5,184,870 |
| Provision for site restoration | 28,101 | 28,101 | 28,101 | 28,101 |
| Term borrowings: Non-current portion | 129,848,494 | 141,567,340 | 129,848,494 | 141,567,340 |
| Deferred tax liability | - | 1,906,850 | - | 1,906,850 |
| | **137,465,758** | **148,662,899** | **137,476,533** | **148,687,161** |
| **Current liabilities** | | | | |
| Lease liabilities | 1,961,187 | 5,833,975 | 1,961,187 | 5,788,769 |
| Term borrowings: Current portion | 47,332,522 | 30,069,355 | 47,332,522 | 30,069,355 |
| Trade and other payables | 50,266,904 | 45,732,759 | 50,185,079 | 45,310,307 |
| Contract liabilities | 4,670,413 | 8,250,357 | 5,030,858 | 8,610,802 |
| Bank overdrafts | 18,946,045 | 23,612,164 | 18,946,045 | 23,612,164 |
| | **123,177,071** | **113,498,610** | **123,455,691** | **113,391,397** |
| **TOTAL LIABILITIES** | **260,642,829** | **262,161,509** | **260,932,224** | **262,078,558** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **388,848,540** | **398,171,928** | **387,958,268** | **396,935,208** |

| Consolidated and separate statements of cash flows for the year ended 30 June 2021 | Group June 2021 TZS'000 | Group June 2020 TZS'000 | Company June 2021 TZS'000 | Company June 2020 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| **Cash generated from operating activities** | | | | |
| Operating (loss)/profit | (5,179,403) | 4,395,339 | (5,210,010) | 4,475,461 |
| Adjusted for non cash items: | | | | |
| Depreciation charge | 11,514,776 | 12,259,025 | 11,489,807 | 12,205,127 |
| Other unrealised charges | 3,296,404 | - | 3,296,404 | - |
| (Decrease)/increase in ECL on bank balances | (2,743) | (186,230) | (2,685) | (184,758) |
| Increase/(decrease) in ECL on trade receivables | 144,243 | 5,767 | 213,060 | (46,786) |
| Bad debts write off | 149,769 | - | 149,769 | - |
| Increase in provision for leave pay | 128,025 | - | 128,025 | - |
| Increase in provision for obsolete inventories | 1,601,725 | - | 1,601,725 | - |
| **Operating profit before working capital changes** | **11,652,796** | **16,473,900** | **11,666,095** | **16,449,044** |
| (Increase)/decrease in inventories - less provisions | (9,837) | 514,563 | (9,837) | 514,563 |
| (Increase)/decrease in trade and other receivables - gross | (1,948,313) | (4,090,185) | (2,273,957) | (4,665,366) |
| Decrease in VAT recoverable | - | - | - | - |
| Decrease in trade and other payables | 4,534,145 | 1,552,912 | 4,874,772 | 1,543,435 |
| (Decrease)/increase in contract liabilities | (3,579,944) | 2,733,739 | (3,579,944) | 2,964,395 |
| Decrease in derivative liabilities | - | (686,824) | - | (686,824) |
| **Cash generated from operating activities** | **10,648,847** | **16,498,105** | **10,677,129** | **16,119,247** |
| Interest income received | 945 | 3,159 | 945 | 3,159 |
| Income taxes paid | (892,766) | (484,410) | (857,129) | (242,789) |
| **Net cash flows from operating activities** | **9,757,027** | **16,016,854** | **9,820,945** | **15,879,617** |
| **INVESTING ACTIVITIES** | | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | (3,823,044) | (997,502) | (3,823,044) | (997,502) |
| Net cash flows used in investing activities | (3,823,044) | (997,502) | (3,823,044) | (997,502) |
| **FINANCING ACTIVITIES** | | | | |
| Principal repayments - lease liabilities | (1,692,257) | (301,207) | (1,668,617) | (271,760) |
| Lease liability interest paid | (424,151) | (29,785) | (421,005) | (21,014) |
| Interest paid - overdrafts | (737,221) | (1,034,907) | (737,221) | (1,034,907) |
| Interest paid - term borrowings | - | (3,481,154) | - | (3,481,154) |
| Principal repayments - term borrowings | - | (12,185,310) | - | (12,185,310) |
| **Net cash flows used in financing activities** | **(2,853,629)** | **(17,032,363)** | **(2,826,843)** | **(16,994,145)** |
| **Net (decrease)/increase in cash and cash equivalents** | **3,080,354** | **(2,013,011)** | **3,171,058** | **(2,112,030)** |
| Net foreign exchange differences | (295,798) | (392,820) | (296,932) | (363,386) |
| Cash and cash equivalents at 1 January | (20,407,592) | (19,259,332) | (20,569,406) | (19,471,196) |
| **Cash and cash equivalents at 30 June** | **(17,623,036)** | **(21,665,163)** | **(17,695,280)** | **(21,946,612)** |

**Information to Members**

The company secretary would like to inform the members that dividends can be directly transferred to their bank

Members can contact The Dar es Salaam Stock Exchange on +255 (0)22 2123983 or on +255 (0)22 2128522 for information on how to have the dividends deposited directly into their bank

**L Masha**
Chairman
30 September 2021

**R Swart**
Managing Director

**Q Ganijee**
Company Secretary

**Tanga Cement Public Limited**
P O Box 5053
Tanga
Tanzania
info@simbacement.co.tz

SYSTEM CERTIFICATION ISO 9001 SGS

216485101

# UMOJA CUP 2021 RORYA KUANZA RASMI JUMAMOSI

**Na Mwandishi Wetu**

MICHUANO maarufu ya Umoja Cup ambayo hutikisa Wilaya ya Rorya kwa upande wa mpira wa miguu na pete kila mwaka, kwa mwaka huu inatarajiwa kuanza kutimua vumbi rasmi Jumamosi wiki hii katika viwanja vya Maji Sota.

Mwenyekiti wa mashindano hayo, Ochieng Melly, akizungumza na mwandishi wetu mapema wiki hii, alisema timu zilizojitokeza kushiriki kwa upande wa mpira wa miguu kwa wanaume ni 20 na mpira wa pete ni sita.

Ochieng alizitaja timu zilizothibitisha kushiriki michuano hiyo ambayo hudhaminiwa na mdau maarufu wa soka wilayani humo, Peter Owino, kuwa ni Shirati Mji FC, Rifa, Watumishi FC, lwala FC, Kirengo, Riangachi, Bweru, Kabwana FC, Bodaboda FC, Wanamaji na Magamaga FC.

Nyingine zilizothibitisha kushiriki michuano hiyo ambayo mbali na bingwa kuzawadiwa kombe pia huibuka na kitita cha Sh. 350,000, mshindi wa pili Sh. 250,000 na mpira huku wa tatu akilamba Sh. 150,000, ni Minigo, Mennonite, Masonga, Bweru, Bubombi, Nyaera, Lolwe, Mtakuja na Kyariko FC.

Aidha, Ochieng alisema mashindano ya mwaka huu yatabeba jina la mchezaji wa Wanamaji FC, aliyefariki hivi karibuni, Makori Odoyo 'Abega wa Cameroon', ambaye anakumbukwa kwa umahiri wake katika kikosi cha timu hiyo kilichoshiriki Ligi ya Mkoa wa Mara akiwa pamoja na Sadi Mato, Bonjo Ochola na wengine wengi chini ya Kocha wao, Charles Kilinda.

Ochieng alisema familia ya Abega ambaye alipewa jina hilo kutokana utaalamu wake dimbani kama walivyokuwa wachezaji wa Cameroon, imekubali Umoja Cup 2021 kumuenzi kijana wao na kuahidi kushiriki katika kufanikisha mchezo wa soka unadumishwa katika timu yake.

Kwa upande wa Kocha wa Wanamaji FC, Godfrey Joseph, alisema: "Ni pigo kubwa kwetu kumpoteza Abega ambaye mazishi yake yalifanyika Septemba 21, mwaka huu, huku akiwa ameacha mke na watoto watatu".

Akizungumzia malengo ya baadaye ya michuano hiyo, Meneja wa Mashidano hayo, Daniel Obong'o, alisema mkakati wao ni kuyafanya yawe makubwa zaidi licha ya kukumbana na changamoto za kifedha kwa kuwa hayana viingilio hivyo kusababisha wachezaji kukosa motisha pamoja na gharama za usafiri.

Obong'o alisema mashindano hayo yamekuwa yakimtegemea tu mdau wa michezo wilayani hapo, Peter Owino 'Jasota', ambaye huyadhamini kwa kutoa zawadi ya pesa taslimu, mipira kombe ngao, vifaa mbalimbali kwa timu tatu za juu na mipira.

"Ni kwa vile mdhamini wetu anasimamia kila kitu, hivyo anaagiza tusiweke kiingilio ili wapenda soka Rorya waweze kuangalia michezo hiyo bure kila mwaka, kwa sababu wakazi wa huku kwetu wanapenda sana mpira," alisema Obong'o.

Naye mdhamini wa mashindano hayo, Owino, alisema lengo la kudhamini michuano hiyo kwa mwaka wa tisa sasa, ni kuhakikisha wakazi wa Rorya wanapata burudani waipendayo ya soka, lakini michuano hiyo ikitumika kuibua vipaji na kujenga undugu.

"Michuano hii huwakutanisha watu pamoja na kujenga undugu, mimi huwa nafarijika kuona Wanarorya wanakuwa wamoja na kujenga ushirikiano, lakini huibu vipaji kwani vijana wengi wamepata ajira kwa kucheza timu kubwa wakitokea katika michuano hii," alisema Owino.

**KIMATAIFA...**



Baadhi ya washiriki wa mashindano ya baiskeli ya kimataifa yatakayojumuisha nchi za Afrika Mashariki, wakipita mbele ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula ( watano kulia) jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa ufunguzi wa mshindano hayo katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Simba yatoa sababu sare Biashara United

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushindwa kuibuka na ushindi kwenye mechi yao ya ufunguzi ya Ligi Kuu Bara, uongozi wa Simba, umesema hawakuwa na bahati katika mchezo wao dhidi ya Biashara United na wanatarajia kufanya vizuri katika mechi zijazo ikiwamo dhidi ya Dodoma Jiji FC itakayopigwa Ijumaa wiki hii.

Simba ambayo ilitoka suluhu dhidi ya Biashara United ya Mara juzi, Ijumaa itakuwa ugenini kuvaana na Dodoma Jiji FC, mchezo utakaopigwa katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Akizungumzia jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema licha ya wachezaji wao kupambana, lakini haikuwa bahati kwao kuondoka na pointi tatu.

Alisema mbali na kutokuwa na bahati, lakini pia uwanja haukuwa rafiki kwao licha ya kubadili mfumo na kucheza mipira mirefu ya juu.

"Tumepokea matokeo, ni sehemu ya mchezo na sasa tunajipanga kwa mechi yetu ijayo dhidi ya Dodoma Jiji FC, kutafuta matokeo chanya," alisema Matola.

Wakati huo huo, Thierry Hitimana, ambaye ni miongoni mwa kocha msaidizi wa timu hiyo, ambaye alibaki jijini akiendelea na programu na wachezaji ambao hawakusafiri na timu, alisema ana matarajio makubwa na Simba kutetea ubingwa wao.

"Bado hatujakaa sawa, mashabiki wanatakiwa kuwa wavumilivu kwa sababu kuna wachezaji wawili wameondoka, hivyo wale waliokuwapo wanahitaji muda wa kuzoeana na kutengeneza kombinesheni na wageni," alisema Hitimana.

Alisema Simba imepata 'Pre Season' (maandalizi ya msimu mpya mazuri, lakini ilikuwa na wachezaji pungufu kutokana na wengi wao kuwa katika majukumu ya timu ya taifa na waliporejea tayari muda wa kambi ulimalizika.

# Biashara United yamulika pia CAF

**Na Saada Akida**

WAKATI wakiwa na kibarua kigumu dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Biashara United, Patrick Odhiambo, amesema ameanza pia kusoma ubora na udhaifu wa wapinzani wao, Al Ahly Tripoli ya Libya kuelekea mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika Oktoba 15, mwaka huu.

Biashara United ambayo juzi ilitoka suluhu dhidi ya Simba katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma, Oktoba Mosi itaikaribisha Ruvu Shooting uwanjani hapo kabla ya mchezo huo wa kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Odhiambo alisema wakati wakihitaji kupata matokeo katika mchezo wa ligi, analazimika pia kufuatilia ubora na udhaifu wa wapinzani wao katika michuano hiyo ya CAF ili kufikia malengo ya kusonga mbele.

Alisema anatambua ligi inaushindani mkubwa, lakini inamlazimu kuhakikisha anasuka kikosi chake kwa kupambana kutafuta matokeo katika mechi hizo pamoja na michuano hiyo ya kimataifa dhidi ya Al Ahly Tripoli.

"Tunahitaji kufanya vizuri katika ligi, lakini kuhakikisha hizi nafasi za timu nne Tanzania kucheza michuano ya kimataifa tusiipoteze, Biashara ikiwa miongoni tuliopewa dhamana hiyo tunalazimika kufanya vizuri.

"Kufanya kwetu vizuri na kuendelea kupata nafasi hiyo adimu tunatakiwa kupambana kupata matokeo mazuri katika michezo yetu," alisema Odhiambo.

Alisema wakati wanatafuta pointi katika michezo ya Ligi Kuu, pia wanatumia nafasi hiyo kuimarisha kikosi chao kukabiliana na Walibya hao.

Kocha huyo alisema anaamini mechi yao dhidi ya Simba pamoja na watakayocheza dhidi ya Ruvu Shooting, itawasaidia kujiimarisha hasa nafasi ya ulinzi kwa sababu wanaenda kukutana Walibya hao ambao wapo vizuri katika safu ya ushambuliaji.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MARTIAL AFUNGIWA KAZI
KLABU ya Borussia Dortmund inafikiria kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa na Manchester United, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 25, kama straika wao raia wa Norway, Erling Haaland, 21, ataondoka katika klabu hiyo msimu wa majira ya joto. **(Sport1)**

### TIELEMANS AGOMBEWA HISPANIA
BARCELONA na Real Madrid zitakuwa miongoni mwa klabu zinazomwania kiungo wa kati wa Leicester, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24, ikiwa kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji atauzwa, msimu ujao. **(Athletic)**

### MCKENNIE AWANIWA WEST HAM
WEST Ham wanashughulikia mpango wa kumsajili kiungo wa Juventus, Weston McKennie mwenye umri wa miaka 23, na mazungumzo tayari yamefanyika juu ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani. **(Football Insider)**

### DANJAMU ATAKIWA LIVERPOOL
WINGA wa zamani wa Bournemouth, Arnaut Danjuma mwenye umri wa miaka 24, anafuatiliwa kwa karibu na Liverpool baada ya Mholanzi huyo kuanza msimu vizuri katika klabu yake mpya ya Villarreal. **(Voetbal International)**

### LIVERPOOL YAMTAKA DIAZ
LIVERPOOL wamekuwa wakimfuatilia kiungo wa kati wa Porto, Mcolombia Luis Diaz mwenye umri wa miaka 24. **(Independent)**

### MAXIMIN KWA CHELSEA, LIVER
CHELSEA na Liverpool zinamnyatia winga wa Newcastle na Ufaransa, Allan Saint-Maximin mwenye umri wa miaka 24. **(Calciomercato via Express)**

### TOTTENHAM KUMUUZA DELE
KLABU ya Tottenham Hotspur huenda ikasubiri hadi msimu ujao badala ya Januari kabla ya kujaribu kumuuza tena, Dele Alli mwenye umri wa miaka 25, ikizingatiwa thamani ya kiungo huyo wa kati wa England ilivyoshuka. **(Football Insider)**

### DENI LA BARCA KUNUNULIWA
BARCELONA wamepokea ofa kutoka kwa Kampuni ya Dubai ya kununua deni la klabu hiyo la euro bilioni 1.5. **(8tv via Mirror)**

### ANTONY KWENYE RADA ULAYA
BARCELONA wameungana na Bayern Munich katika kinyang'anyiro cha kumsaka winga wa Ajax, Antony mwenye umri wa miaka 21 raia wa Brazil. **(Sport)**

### SANE, PULISIC HATAPISHANA
CHELSEA na Bayern Munich kwa sasa hawana mpango wowote wa kubadilishana wachezaji kati ya winga wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 23, na winga, Leroy Sane, 25, licha ya uvumi unaoendelea. **(Fabrizio Romano)**

### MOURINHO AMTAKA NDOMBELE
KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, anaitaka huduma ya kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 24 katika klabu hiyo. **(Calciomercato via FourFourTwo)**

### FEKIR KUONGEZA MKATABA
REAL Betis wameanza mazungumzo ya kurefusha mkataba wa mshambuliaji wa Ufaransa, Nabil Fekir mwenye umri wa miaka 28. **(Marca)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AFUNGUKA BAO LAKE LA KWANZA PSG

Kadri tunavyocheza pamoja na Neymar na Mbappe, tutazidi kuwa bora zaidi, tunatakiwa kukua pamoja, kuongeza...

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi amesema kwamba, upatina wake na Neymar na Kylian Mbappe, utaimarika zaidi hapo Paris Saint-Germain kadri wanavyocheza pamoja kila wakati.

Messi amebainisha hayo baada ya kufunga bao lake la kwanza kwa PSG juzi, Jumanne wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Manchester City kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Raia huyo wa Argentina, hakuwa na mwanzo mzuri baada ya kushindwa kufunga kwenye mechi tatu za kwanza tangu alipojiunga na timu hiyo kwa mkataba wa miaka miwili baada ya kuondoka kule Barcelona, lakini Jumanne alikuwa na wakati mzuri.

Baada ya kipindi cha kwanza kilichojaa purukushani nyingi, mshambuliaji huyo alicheza vizuri na Mbappe na akafunga bao dakika ya 74 kwa mkwaju mkali kutoka nje ya 18.

"Nina furaha kubwa kufunga," alisema Messi, nimerudi uwanjani baada ya kukaa nje kwenye mechi mbili kutokana na kuumia goti.

"Sijacheza sana hivi karibuni. Mchezo mmoja tu (kwenye dimba la Parc des Princes), na huu ni wa pili hapa. Kwa hakika naanza kuzoea timu mpya na wachezaji wenzangu.

"Kadri tunavyocheza pamoja (Neymar na Mbappe), tutazidi kuwa bora zaidi. Tunatakiwa kukua pamoja, kuongeza kiwango cha kucheza, tulicheza vizuri. Tumejitoa kwa ubora wetu na tutaendelea kufanya hivyo."

Bao lake liliwafanya mashabiki hapo kwenye Uwanja wa Parc des Princes kulipuka kwa shangwe kubwa pamoja na kocha, Mauricio Pochettino.

"Nimetumia miaka 20 kumwangalia yeye akifunga mabao kutoka sehemu tofauti za uwanja na hii ni mara ya kwanza anaifungia timu hii na hivyo natakiwa kushangilia," alisema Pochettino huku akitabasamu.

"Unahitaji aina hii ya kiwango cha wachezaji kama yeye na unahitaji yeye kujihisi vizuri baada ya kufunga.

"Sasa anahitaji kutengeneza uhusiano mpya na timu nyingine baada ya miaka 20 akicheza kule Barcelona.

"Kwa sasa anajihisi tofauti, kuna hisia nyingi sana kwa upande wake yeye."

MECHI KALI
HOME
AWAY
CELTIC
3.60 | 3.75 | 1.94
BAYER LEVERKUSEN

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 537

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MADRID HAIKUSTAHILI KUFUNGWA - ANCELOTTI



**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema hawakustahili kupoteza mchezo wao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya "wakuja' Sheriff.

Sheriff ni timu kutoka nchini Moldova ambayo inashiriki michuano hiyo kwa mara ya kwanza katika historia yake, iliwashitua wenyewe kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu kwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 juzi, Jumanne.

Jasurbek Yakhshiboev alifunga bao la ufunguzi kwa kichwa kipindi cha pili, kabla ya Karim Benzema kuisawazisha Madrid kwa mkwaju wa penalti.

Lakini Sebastien Thill alipeleka kilio kwa Madrid wakati alipofunga katika dakika ya 89 na kuiwezesha timu hiyo iliyoanzishwa mwaka 1997 kupata ushindi wa kihistoria.

'Los Blancos' hao walipiga mashuti 31 na 11 kati yake yakilenga lango na walikuwa na utawala wa mchezo wa asilimia 75, huku Sheriff ikipiga mashuti manne tu, lakini waliondoka na pointi zote tatu kwenye mji huo mkuu wa Hispania.

Matokeo hayo yameiacha Madrid kwenye nafasi ya pili katika Kundi lake la D, wakipitwa pointi tatu na Sheriff, ambapo sasa wameshinda mechi tatu za mashindano hayo.

"Zaidi ya kuogopa, tuna huzuni sana," alisema Ancelotti baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulicheza kwa bidii yote na tulionekana kuwa vizuri, lakini tumepoteza mchezo muhimu sana kwetu, ingawa nao walicheza vizuri tu.

"Hatukuwa vizuri kwenye umaliziaji, kwa kweli ni ngumu sana kuelezea hali hii kwa sasa.

"Ni vitu vidogo tu vilitugharimu sisi kwenye mchezo huu. Ni somo zuri sana kwetu katika mechi zinazokuja, kwa sababu hatukustahili kupoteza."

Madrid itacheza na Shakhtar Donetsk ugenini Oktoba 19 kwenye mchezo wao ujao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# SportPesa yasaini mkataba wa matangazo na Mdundo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya SportPesa Limited, inayoongoza kwa michezo ya ubashiri katika michezo aina mbalimbali, imesaini mkataba wa matangazo wa muda mrefu na Kampuni ya Matangazo ya Mdundo ya nchini Tanzania yenye wafuatiliaji zaidi ya milioni 9.7.

Kwa kuanzia kampuni hizo zimesaini mkataba wa mwaka mmoja, ambapo ndani ya mkataba huo wenye thamani ya dola za Marekani 100,000, kampuni ya SportPesa itawasilisha matangazo yake zaidi ya 600 ya sauti yakitarajiwa kuwafikia zaidi ya watumiaji milioni 9.7 wa Mdundo.

Mkataba huu ni ushahidi dhahiri ya ubunifu mkubwa unaofanywa na Kampuni ya Mdundo wenye malengo ya kuwafikia na kuwaridhisha wateja wake haswa ikitiliwa maanani ya kuwa pia imeingia mikataba na kampuni nyingine zenye mafanikio makubwa yakiwamo Standard Chartered, Nivea, 9mobile, Safaricom, Coca-Cola, Guinness, Airtel, Vodacom, Carrefour Supermarket na Diageo.

Hivi karibuni Kampuni ya Mdundo pia iliingia mkataba wa matangazo kupitia midundo ya muziki na kampuni za Airtel Nigeria, MTN Nigeria na Vodacom Tanzania, ambapo Mdundo imechangia kwa kiasi kikubwa kwa kampuni hizo kuwafikia walengwa wengi kupitia ubunifu wake.

Mkuu wa kitengo cha chapa za biddhaa wa Kampuni ya Mdundo.com, Rachel Karanu, alisema: "Kujenga mazingira mazuri ya thamani ya kibiashara ya bidhaa za wateja wetu ndiyo msingi muhimu wa kampuni yetu na ambayo yatakuwa endelevu. SportPesa ni taasisi yenye wabunifu na wenye mawazo yenye umakini mkubwa kwa malengo ya kupata matokeo chanya; matarajio yetu ni kufanya kazi na timu yenye malengo ya matokeo chanya iliyoko Sportpesa".

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya SportPesa Tarimba Abbas, kwa upande wake alisema: "Tumefurahi sana kwa kuanza kufanya kazi na Kampuni ya Mdundo.com kupitia mradi huu, hasa ikitiliwa maanani mafaniko ambayo taasisi zingine zimeshapata kupitia ubunifu wa Kampuni ya Mdundo.com".

## HABARI MICHEZO

7,737,060

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 02.10.21 | 17:00 | Derby vs Swansea | 2.52 | 3.22 | 2.72 |
| 2. 02.10.21 | 17:00 | Peterborough vs Bristol City | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 3. 02.10.21 | 17:00 | Luton Town vs Huddersfield | 2.39 | 3.25 | 2.86 |
| 4. 02.10.21 | 17:00 | Hull City vs Middlesbrough | 2.86 | 3.25 | 2.39 |
| 5. 02.10.21 | 17:00 | Blackpool vs Blackburn | 2.86 | 3.16 | 2.45 |
| 6. 02.10.21 | 17:00 | Barnsley vs Millwall | 2.27 | 3.20 | 3.11 |
| 7. 02.10.21 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.40 | 3.47 | 2.78 |
| 8. 02.10.21 | 19:30 | Brighton vs Arsenal | 2.85 | 3.15 | 2.58 |
| 9. 02.10.21 | 22:00 | Atletico Madrid vs Barcelona | 2.14 | 3.32 | 3.47 |
| 10. 03.10.21 | 16:00 | Tottenham vs Aston Villa | 2.14 | 3.46 | 3.36 |
| 11. 03.10.21 | 16:00 | Crystal Palace vs Leicester | 3.21 | 3.46 | 2.20 |
| 12. 03.10.21 | 18:00 | Lille vs Marseille | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 13. 03.10.21 | 18:30 | Liverpool vs Manchester City | 2.75 | 3.39 | 2.52 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 30 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2755 | Khimki M vs Kolomna | 1.40 | 4.47 | 6.41 |
| 15:30 | 1847 | AL Ahed vs Shabab EL Bourj SC | 1.99 | 3.33 | 3.43 |
| 15:30 | 5466 | Catania vs Torre Neapolis | 1.95 | 3.22 | 4.06 |
| 16:00 | 4704 | KF Dukagjini vs KF Drita | 4.50 | 3.60 | 1.78 |
| 16:00 | 5358 | Shabab AL Khaleel vs Thagafi Tulkarem | 1.14 | 6.76 | 14.48 |
| 16:00 | 5676 | FC Prishtina vs KF Ulpiana | 1.41 | 4.33 | 6.55 |
| 17:30 | 1133 | Radnicki Nis vs Metalac | 1.95 | 3.48 | 3.38 |
| 18:00 | 2676 | Znamya vs Dynamo II | 4.74 | 3.87 | 1.60 |
| 18:00 | 4520 | AL Salt vs Sahab Club | 1.39 | 4.16 | 7.35 |
| 18:30 | 2126 | Haka vs Hifk | 2.52 | 2.91 | 2.81 |
| 18:30 | 2596 | Al Raed Club vs Dhamk | 2.15 | 3.65 | 3.01 |
| 18:35 | 5816 | Abha vs Al Nasr Riyadh | 6.94 | 4.76 | 1.40 |
| 19:45 | 1578 | Lyon vs Brondby | 1.22 | 6.40 | 11.99 |
| 19:45 | 1780 | Zorya Lugansk vs Roma | 7.00 | 4.60 | 1.43 |
| 19:45 | 1814 | Fenerbahce vs Olympiakos | 2.33 | 3.19 | 3.14 |
| 19:45 | 2005 | Legia Warszawa vs Leicester | 5.00 | 3.95 | 1.65 |
| 19:45 | 2147 | Royal Antwerp vs Eintracht Frankfurt | 3.79 | 3.84 | 1.87 |
| 19:45 | 2517 | Alashkert Martuni vs HJK Helsinki | 3.56 | 3.21 | 2.14 |
| 19:45 | 2606 | Napoli vs Spartak Moscow | 1.25 | 5.99 | 10.98 |
| 19:45 | 2672 | Sparta Prague vs Rangers | 2.64 | 3.29 | 2.64 |
| 19:45 | 3293 | Real Sociedad vs Monaco | 2.24 | 3.50 | 3.05 |
| 19:45 | 4281 | Partizan vs Flora Tallinn | 1.19 | 6.62 | 14.04 |
| 19:45 | 4682 | AZ Alkmaar vs Baumit Jablonec | 1.41 | 4.80 | 7.00 |
| 19:45 | 5158 | KAA Gent vs Anorthosis Famagusta | 1.44 | 4.60 | 6.79 |
| 19:45 | 5374 | Sturm Graz vs PSV Eindhoven | 4.50 | 4.00 | 1.70 |
| 19:45 | 5402 | CFR Cluj vs Randers | 1.86 | 3.54 | 4.19 |
| 19:45 | 5536 | CSKA Sofia vs Bodo Glimt | 2.56 | 3.41 | 2.66 |
| 19:45 | 5987 | LASK Linz vs Maccabi Tel Aviv | 2.06 | 3.55 | 3.40 |
| 20:00 | 1311 | AFC Eskilstuna vs Osters IF | 2.65 | 3.15 | 2.75 |
| 20:00 | 2780 | IFK Varnamo vs Vasteras SK | 1.82 | 3.54 | 4.39 |
| 20:00 | 3841 | IK Brage vs Vasalunds IF | 1.84 | 3.80 | 3.95 |
| 20:30 | 5472 | AL Aqaba vs FC Maan | 1.88 | 3.10 | 4.16 |
| 22:00 | 1434 | Lazio vs Lokomotiv Moscow | 1.34 | 5.19 | 8.38 |
| 22:00 | 1472 | Curico Unido vs Cobresal | 2.46 | 3.28 | 2.61 |
| 22:00 | 1522 | Ludogorets Razgrad vs Red Star Belgrade | 2.35 | 3.45 | 2.90 |
| 22:00 | 1919 | Racing Genk vs Dinamo Zagreb | 2.08 | 3.35 | 3.55 |
| 22:00 | 1986 | FC Basel vs Kairat Almaty | 1.42 | 4.80 | 6.80 |
| 22:00 | 2351 | Tottenham vs NK Mura | 1.11 | 8.61 | 23.02 |
| 22:00 | 2539 | Vitesse Arnhem vs Rennes | 3.20 | 3.45 | 2.18 |
| 22:00 | 2709 | PAOK vs Slovan Bratislava | 1.35 | 4.88 | 8.70 |
| 22:00 | 2945 | Ferencvaros TC vs Betis | 4.90 | 3.95 | 1.66 |
| 22:00 | 2974 | Copenhagen vs Lincoln FC | 1.08 | 9.65 | 30.95 |
| 22:00 | 4183 | Union Berlin vs Maccabi Haifa | 1.45 | 4.59 | 6.59 |
| 22:00 | 4230 | Marseille vs Galatasaray | 1.63 | 4.18 | 4.78 |
| 22:00 | 4479 | Sporting Braga vs Midtjylland | 2.02 | 3.36 | 3.76 |
| 22:00 | 4518 | Avellino vs Catanzaro | 2.42 | 3.02 | 3.07 |
| 22:00 | 4562 | Feyenoord vs Slavia Prague | 2.03 | 3.65 | 3.40 |
| 22:00 | 4827 | West Ham vs Rapid Vienna | 1.25 | 5.99 | 10.98 |
| 22:00 | 5054 | Omonia Nicosia vs Karabakh | 2.55 | 3.21 | 2.80 |
| 22:00 | 5087 | Celtic vs Bayer Leverkusen | 3.60 | 3.75 | 1.94 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# ITALIA, ARGENTINA KUVAANA JUNI 2022



**LONDON, Uswisi**

ITALIA itacheza na Argentina Juni 2022, baada ya Shirikisho la Soka la Ulaya (UEFA) na lile la Amerika Kusini (CONMEBOL), kukubaliana kuwa na mechi kati ya mabingwa wa Ulaya na Copa America.

Italia ni mshindi wa Euro 2020, ambapo walisubiri kwa miaka 53 kubeba taji hilo, wakati walipowafunga England, kwenye fainali Julai na watacheza na mabingwa wa Copa America 2021, Argentina, mwakani.

Huku uwanja bado ukiwa haujapangwa, kwa ajili ya mchezo huo, pia kutakuwa na mechi nyingi zaidi kati ya washindi wa mabara hayo mawili kwa miaka inayofuata.

Taarifa kutoka mashirikisho hayo mawili ilisema: "UEFA na CONMEBOL leo (jana) zinatangaza kwamba, zimefikia makubaliano ya ushirikiano kwa kuandaa mchezo kati ya mshindi wa UEFA Euro 2020 Italia na mshindi kutoka CONMEBOL Copa America 2021, Argentina, wakati wa dirisha la mechi za kimataifa Juni 2022 katika uwanja utakaotangazwa.

"Kuandaa kwa mchezo huu ni sehemu ya kupanua ushirikiano kati ya UEFA na CONMEBOL, ambapo utahusisha soka la wanawake, vijana na kubadilishana waamuzi, pamoja na mafunzo.

"Makubaliano yamefikia kati ya mashirikiano haya mawili kwa sasa, kwa ajili ya mechi ya mabingwa kutoka mashirikisho haya mawili na tunatarajia kufungua ofisi ya pamoja itakayokuwa na makao makuu yake jijini London, England."

Kufikiwa kwa makubaliano kati ya mashirikisho hayo mawili ni sehemu ya kupinga wazo la Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), ambalo linapanga kujadili mpango wa michuano ya Kombe la Dunia kufanyika kila baada ya miaka miwili badala ya miaka minne ya sasa.

Wazo hilo ambalo litajadiliwa na Fifa, lilitolewa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Soka duniani, Arsene Wenger.

# Guardiola amvulia kofia Donnaruma




**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema muda mwingine unashinda na wakati mwingine unapoteza, lakini golikipa wa PSG, Gianluigi Donnaruma, alifanya kazi yake kwa kuokoa hatari nyingi.

Man City ilifungwa mabao 2-0 na PSG, kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumanne wakati Lionel Messi akifunga bao lake la kwanza kwa timu hiyo ya Paris tangu atue hapo akitokea Barcelona.

Baada ya mchezo huo, Guardiola alisema kupoteza kwao, mchezo wa Ligi ya Mabingwa mbele ya PSG ni moja ya vipindi, ambavyo vinatokea kwenye mpira, hivyo wanakwenda kula vizuri na kupumzika, kwa ajili ya mchezo wao ujao, dhidi ya Liverpool kwenye Ligi Kuu England.

Guardiola alisema walicheza kwa mbinu za kusaka ushindi, lakini kilichotokea ni uimara wa kipa wa PSG, Donnaruma ambaye alifanya kazi kubwa kwenye kuokoa hatari za wachezaji wake.

"Tulikuwa tunahitaji ushindi na tumecheza namna hiyo, lakini ni sehemu ya matokeo na huwa inatokea kwenye soka. Yote kwa yote kipa wa PSG Donnaruma alifanya kazi yake kwa kuokoa hatari nyingi. "Kwa matokeo, ambayo yametokea hamna namna tunakwenda kupumzika vizuri, kutafuta chakula na kula vizuri pamoja na kupata muda wa kumpumzika, kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu, dhidi ya Liverpool," alisema.

Jumapili wiki hii, Man City iliyopo nafasi ya pili, kwenye msimamo wa Ligi Kuu na pointi zake 13, itakutana na Liverpool, ambayo ni vinara wakiwa na pointi 14, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Anfield.

# Michezo

Alhamisi Septemba 30, 2021

Nipashe





Guardiola amvulia kofia Donnaruma UKURASA 23

KAZI KWELI!...




Straika wa Kagera Sugar, Meshack Abraham (juu) akiwania mpira na beki wa Yanga, Yannick Bangala, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoka jana. Yanga ilishinda 1-0. NA MPIGAPICHA WETU

# Yanga ya moto aisee

## Fei Toto aendeleza maajabu akiipa pointi 3 dhidi ya Kagera Sugar, KMC yapigishwa kwata Polisi kwa...

**Na Adam Fungamwango**

YANGA haitaki kupoa! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya kuendeleza dozi ya bao 1-0 kwa kuifumua Kagera Sugar nyumbani ikiwa ni siku nne tu tangu ilipotoa adhabu kama hiyo kwa watani wao wa jadi, Simba.

**Watani hao wa jadi walikutana Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Jumamosi iliyopita kwenye mechi ya Ngao ya Jamii maalum kwa ajili ya kuukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Bara 2021/22 na Simba kukubali kipigo cha bao 1-0**

Hata hivyo, jana ikicheza ugenini katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoka, uzembe wa kiungo mkabaji Jackson Kibirige wa Kagera Sugar, uliiwezesha Yanga kuendeleza moto wao kwa kuondoka na pointi zote tatu kwa ushindi wa bao 1-0, ikiwa ni mechi yao ya kwanza msimu huu wa Ligi Kuu Bara.

Kibirige akiwa kwenye eneo la hatari, alitaka kupiga chenga golini na mpira ulinaswa na wachezaji wa Yanga, Fiston Mayele akiachia shuti kali lililopanguliwa na kipa Ramadhani Chalamanda, kabla ya kurejea uwanjani na kumkuta Feisal Salum 'Fei Toto' aliyeukwamisha mpira wavuni dakika ya 23 ya mchezo.

Ulikuwa ni ushindi wa kwanza kwa Yanga kwenye mechi ufunguzi baada ya misimu miwili. Msimu wa mwisho Yanga kushinda mechi ya ufunguzi ilikuwa ni 2018/19 ilipoifunga Mtibwa Sugar mabao 2-1, lakini 2019/20 ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting na msimu uliopita, ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons.

Awali, baada ya mpira kuanza, iliwachukua Yanga dakika saba tu kupiga hodi kwenye lango la Kagera Sugar, kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Mayele, mpira ukamkuta Fei Toto akiwa kwenye eneo la hatari, akaachia shuti la mguu wa kushoto lililotoka nje sentimeta chache.

Ikiendelea kulishambulia lango la wenyeji wao, Yanga ilipata nafasi nyingine dakika mbili baadaye, Yacouba Songne aliachia shuti kali lililotoka nje.

Yacouba aliendelea kukosa magoli dakika ya 25 na 45, akiwa anatazamana na kipa Chalamanda, ambaye alikuwa shujaa kwa kupangua mikwaju hiyo, huku timu yake ya Kagera Sugar ikishindwa kufanya shambulio lolote la maana kipindi cha kwanza.

Timu zote zilifanya mabadiliko kipindi cha pili, Yanga ikiwatoa Farid Mussa, Jesus Moloko, Mayele, Yacouba na Fei Toto, nafasi zao zikichukuliwa na Deus Kaseke, Zawadi Mauya, Ditram Nchimbi, Heritier Makambo na Abdallah Shaibu 'Ninja'.

Lakini kuingia kwa Nassor Kapama badala ya Hassan Mwaterema kuliifanya Kagera Sugar kutawala kwa muda mrefu kipindi cha pili, hata hivyo, walishindwa kuipenya ngome ya Yanga ikiongozwa na Yannick Bangala ambaye alisimama imara.

Kwingineko katika Uwanja wa Karatu, wenyeji Polisi Tanzania nao waliianza vema Ligi Kuu kwa kuichapa KMC FC mabao 2-0, shukrani kwa Vitalis Mayanga aliyetupia yote mawili.

# Sababu Mo Dewji kujiuzulu Uenyekiti

**Na Adam Fungamwango**

MWEKEZAJI wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, ametangaza kujiuzulu rasmi katika nafasi yake ya Uenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi huku akimteua kiongozi wa zamani wa klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again' kuchukua kukalia kiti hicho.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Dewji amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa Simba kuwa bado yupo kwenye klabu hiyo, lakini kwa sasa atabaki kuwa mwekezaji kwani ana hisa asilimia 49 kwenye klabu hiyo, pia yeye bado ni mwanachama na shabiki wa Simba hadi siku yake ya mwisho.

Alisema kujiuzulu kwake, kunatokana na yeye mara kwa mara kuwa nje ya nchi, hivyo kukosa muda wa kushughulikia masuala ya klabu ya Simba, hivyo anamteua mtu ambaye atakuwa muda mwingi yupo nchini na kufanya kazi hizo.

Kujiuzulu kwa bilionea huyo kijana Afrika, kunakuja siku moja baada ya Simba kuanza vibaya kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, ikibanwa kwa suluhu bila kufungana dhidi ya Biashara United kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Pia kuna siku chache baada ya kupoteza mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya watani zao wa jadi, Yanga kwa bao 1-0, Uwanja wa Benjamin Mkapa. Hata hivyo, Dewji alisema kuwa maamuzi ya yeye kujiuzulu yalifanyika kwa pamoja katika kikao walichokaa Septemba 21, mwaka huu.

"Muda umefika mimi kama Mohamed kujiuzulu, tumefanya mkutano Septemba 21, mwaka huu, na tumekubaliana kuwa mimi nitajiuzulu kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Simba. Naomba sana msifikirie kwamba mimi nitaondoka Simba. Mimi bado mwekezaji, nina hisa na ninaipenda Simba, nitaendelea kuipenda hadi siku yangu ya mwisho.

"Tumekubaliana kwa kuwa mimi muda mrefu sipo nchini, ninasafiri sana, tunahitaji Mwenyekiti wa Bodi wa kuiongoza klabu hii ambaye uwapo wake ni muhimu sana," alisema Mo na kuongeza.

"Kwa makubaliano ambayo tunayo kati ya mimi mwekezaji na klabu ya Simba, namteua Salim Abdallah Mohamed 'Try Again' kuwa Mwenyekiti mpya wa Bodi ya Klabu ya Simba. Huyu ni mzoefu na ameshawahi kuiongoza klabu hii," alisema.

Mo aliwashukuru wajumbe wa bodi, viongozi wa klabu, wanachama, wapenzi na mashabiki wa Simba kwa kumuunga mkono kwa kipindi chake chote ambacho alikuwa mwenyekiti na kuwa cha mafanikio makubwa kiasi cha kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mara mbili na kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara mara nne.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >